# *HUNA BUDI KUZALIWA MARA YA PILI*

. . .Asuhuhi ya Mkesha wa mwaka, katika ibada ya Bwana. Nami pamoja na Ndugu Neville tulikuwa tukijaribu kukutana, nasi tulikutana, tupate kuzungumzia, yale tungefanya. Nilikuwa nikijaribu kumfanya aje hapa na kuwahubiria ninyi nyote asubuhi ya leo, na kuniacha nihubiri usiku wa leo, kwa hiyo ikawa haikuwezekana, ninayo asubuhi ya leo pamoja na usiku wa leo. Kwa hiyo, yeye ni mwuzaji mzuri. Na kwa hiyo kabla hatujawa na. . .hatujaanza darasa, nilimwambia tungekuwa tu na darasa, kama vile hatukuwa wengi sana hapa asubuhi ya leo, na ili tu kuwa na darasa. Kabla sijafanya hivi, ningetaka kufanya tangazo dogo. Nina. . .

2 Tunao watu waliokuja hapa kutoka New York, kukaa pamoja nasi. Nadhani sikukutana na hao watu. Ndugu Neville alisema ndio kwanza azungumzie hilo. Jana usiku nilisikia kwamba walikuwa na. . .trela lao lilikuwa limeshika moto na kuliharibu trela lao. Nilitoka kwenda kuwaona hao watu, nao walionekana ni Wakristo wazuri, wa kupendeza. Nao, kidogo ni watu maskini, kama tulivyo sisi sote, naye Ndugu Wood na wawili ama watatu wetu tulikuwa tukutane tuone kama tusingeweza kuwanunulia tu trela lingine. Nao walikuwa ni wazuri sana na wakasema. . .bima waliyokuwa wameliwekea, walikuwa wamefikia mahali pagumu ikawalazimu kuachana na hiyo bima. Lakini, hata hivyo, wakala alikuwa ameilipia hiyo bima, ama, nao wakapata—wakarejeshewa bima ya trela lao, ambayo labda itaweza kuwapa trela lingine tena mahali pa hilo. Watajua hilo, nafikiri, Jumatatu ama Jumanne, ama kitu kama hicho, ama Jumanne, ninaamini ndivyo. Na kwa hiyo tunataka ku—kushiriki huzuni yao, kufanya yote tuwezayo ku—kuwasaidia, kuwafahamisha ya kwamba sisi—sisi ni ndugu na dada katika Kristo Yesu, nasi tunahurumiana sisi kwa sisi. Na—nami nafikiri ya kwamba kila mmoja angetaka kujisikia hivyo, kuwapa msaada kidogo wakati huu. Kidogo si kawaida, nafikiri, kamwe sijawahi kuchukua matoleo maishani mwangu, basi ni—nitamwomba Ndugu Neville kufanya hivyo. Hiyo—hiyo ilikuwa ni kulirusha mbali, sivyo? Ni sawa. Asante, Ndugu Ben. Mtu fulani tu, kile, kitu fulani kidogo tu ulicho nacho ambacho ungewapelekea, nina hakika kingethaminiwa.

Ndugu Neville, njoo hapa. Sijui jinsi ya kulifanya. Fanya tu kile unachowazia.

[Ndugu Neville anasema, “Asante, Ndugu Branham. Nami

nafurahia kufanya jambo kwa njia hii, kwa sababu hili ndilo linalotusaidia kuwa zaidi kama Kristo na wa kiroho. Wakati mwingine watu husema, 'Nataka uniombee nipate kuwa Mkristo bora zaidi.' Vema, mimi . . . tayari nimekuombea, sasa nitakuonyesha jinsi ya kuwa mmoja. Amina. Hiyo ndiyo njia ya kulifanya, na kuzifungulia huruma zako. Pia ninajua ya kwamba, Ndugu Elliott, yeye haombi huruma kwa ajili yake, lakini yeye ni kiwete, na kwa hiyo . . . naye amekuwa bila kazi. Kwa hiyo tutaninii tu, asubuhi ya leo, tutaifungua mioyo yetu na kuwasaidia jamaa hawa. (Ninaamini, hizi hapa sahani za matoleo, *hapa*. Naam.)—Mh.]

["Baba wa Mbinguni, asubuhi ya leo, tunakutazamia Wewe, tunapolipokea hili; tukijiangalia wenyewe, jinsi ambavyo Wewe umetubariki sisi sote, na kutupa sisi mali hizi zinazohitajika kwa ajili ya faida na ustawi wetu. Kwako Wewe, asubuhi ya leo, tunatoa haya ambayo tunatoa kama sehemu ndogo ya huruma zetu. Huruma Zako ni kuu!"] Naam. ["Bali, Bwana, tunalithamini kama tungekuwa tu na huruma kidogo, kwa kuwa Wewe umekuwa na huruma nyingi sana kwetu. Hawa hapa wapendwa hawa hapa miongoni mwetu, Mungu, nasi asubuhi ya leo tunaomba ya kwamba Wewe sasa utatubariki tunapoifungua mioyo yetu. Na Wewe uichukue, ufanye jinsi Wewe ungeona ni vema sana kwa Roho Wako. Katika Jina la Yesu, na kwa ajili Yake. Amina."] Amina.

[Ndugu hao wanachukua kama dakika nne kupitisha visahani vya matoleo, wakipokea matoleo ya kusanyiko kwa ajili ya familia ya Elliott, huku mpiga piano anapocheza nyimbo kadhaa.]

3 Nilifikiria, labda, wakati wakifanya jambo hilo, ingenipa nafasi kidogo kuchukua kitu fulani cha kuzungumzia asubuhi ya leo, kutoka kwenye maskini vifungu vya maneno na kadhalika nilivyokuwa nimeandika kwenye kipande cha karatasi. Nadhani wahubiri wote hufanya hivyo. Jina la watu hawa ni lipi, sasa, waliochomekewa na trela? [Ndugu Neville anasema, "Elliott."—Mh.] Elliott. Hivi Ndugu na Dada Elliott na mwanao wamo humu jengoni asubuhi ya leo? Wakiwapo, iwapo mngependa kusimama tu, na kusema, semeni hata kama ni "Tunawashukuru kwa ajili ya . . . " kwa hawa watu, mbona, vema. Mna neno mnalotaka kusema, Ndugu Elliott ama Dada Elliott, na kwa hawa watu? [Ndugu Elliott anaelezea shukrani zao.] Mungu akubariki, Ndugu Elliott. Hilo ni sawa kabisa. Asanteni. Mungu awe pamoja nawe, wewe na Dada Elliott na mwanao.

4 Hao watu wanatoka New York. Sikujua walikuwa hapa. Walisema nilikuwa nao kwenye mahojiano, ama au niliomba pamoja nao ama kitu fulani, wakati mmoja. Sikuwajua mpaka nilipokutana nao jana, na kuwaona kuwa ni Wakristo wa kupendeza, watu wazuri sana. Nao waliishi huko New York, huko juu kwenye Bonde la Mto Hudson mahali fulani, na

labda kupitia kanda ama kitu fulani, wakauamini Ujumbe, nao wakauza yote, wakaja humu, wakitoa tu maisha yao na wakati wao kwa Kristo. Nasi tunawatakeni mjue huu ni wonyesho wetu mdogo, Ndugu na Dada Elliott, kwamba sisi ni wapitaji, pia. "Sisi ni wasafiri na wageni katika ulimwengu huu. Tunautafuta mji ambao Mjenzi na Mbuni wake ni Mungu." Ndipo wakati msiba ulipowapata juu ya mambo haya, wa ibilisi akijaribu kuwateketeza na kuwaogopesha mwondoke, tuko pamoja nanyi asilimia mia moja, kusimama nyuma yenu katika kila kitu tunachoweza kufanya kuwasaidia mpate kujitegemea tena. Msimame katika Jina la Bwana Yesu na muanze kusonga mbele. Msi—msife moyo, la. "Mateso ya mwenye haki ni mengi, lakini Mungu humwokoa kutoka kwa hayo yote." Na kwa hiyo sisi—sisi tunajua tunayatarajia mambo haya kutukia, bali tunajua kwamba pia tunamtazamia Mwokozi wetu Ambaye ni zaidi ya mshindi, sisi tuko, ndani Yake Yeye aliyetukomboa.

5 Sasa, leo kwa namna fulani ni siku nzima, na asubuhi ya leo nilikuwa nikiwazia pale, niliwazia tu ningefundisha kidogo katika darasa la shule ya Jumapili. Kama vile, kulifanya darasa la shule ya Jumapili kutokana nalo asubuhi ya leo. Na usiku wa leo kwenye saa moja na nusu, nataka, yakiwa ni mapenzi ya Mungu, kuleta Ujumbe wangu—wangu wa Mwaka Mpya, kama vile Jumapili iliyopita ama Jumapili usiku nilivyouleta Ujumbe wangu wa Krismasi. Basi usiku wa leo nitauleta Ujumbe wangu wa Mwaka Mpya kwenye saa moja u nusu, Bwana akipenda. Ndugu Neville atakuwa na Ujumbe wake wa Mwaka mpya, nami ninamwona Ndugu Stricker hapa na Ndugu Collins, na, loo, wahudumu wengine huku, naye Ndugu Palmer yupo hapa juu pamoja nasi, kutoka Georgia, na—na wengine mbalimbali huku. Ni wahudumu, mtasikia kutoka kwao usiku wa leo.

6 Basi nilimwita Ndugu Neville jana, na juu ya jambo fulani lililougusa moyo wangu, nikiona kuwa huu ni wa Mwaka Mpya, na pia ni wa kwanza, kama vile Jumapili ya kwanza, mbona, usiku wa leo, badala ya kuwa na mkusanyiko mkubwa na kupiga makelele na kuendelea kama walimwengu wengine wafanyavyo, hebu tule ushirika kwenye usiku wa manane. Mnaona? Mnaona, kumtumikia Bwana. Ndugu Neville alikubali ya kwamba alifikiri lingefaa sana. Basi usiku wa leo, Bwana akipenda, nitagawa ushirika saa sita usiku wa leo. Ndipo tutaanza Mwaka Mpya, sio kwa kupiga makelele na kuendelea, ambalo ni sawa iwapo wanataka kufanya hivyo, lakini hebu tulifanye takatifu zaidi na aminifu, na tuukaribie mwaka huu katika njia ya unyofu kwa Kristo, tukitoa yote tuliyo nayo, na ahadi yetu. Sio kufungua ukurasa mpya ama kitu kama hicho, kuanza mwaka mpya, hatuamini katika upuuzi huo. Unafungua tu ukurasa mpya upate—upate kuulipua kesho yake, kwa hiyo hebu na tuyatoe tu maisha yetu Kwake, na kula ushirika usiku wa leo kwenye usiku wa manane. Nami naamini hiyo ndiyo

mara ya kwanza ninayokumbuka, tangu nimekuwa mhudumu, kupata kufanya hivyo. Unalikumbuka, Ndugu Neville? Lakini jambo jipya kwetu sasa, na ni kwa nadra sana Mwaka Mpya huja jinsi hii, mwajua, kwa hiyo li—lilinishangaza tu, nami nikafikiri lingekuwa ni la kushangaza sana.

7 Nadhani basi huu utakuwa ni kama wakati wa mwisho nitakaoweza kuzungumza nanyi nyote kwa muda fulani sasa, tukiingia katika Mwaka Mpya, tukiingia hudumani, katika utumishi wa Bwana. Nitaondoka yapata juma lijalo, ama mwanzoni mwa juma lifuatalo, kwenda Phoenix, kwa yapata mikutano kumi na mitano, kumi na sita mfululizo, kotekote mabondeni, na kupitia Sunny Slopes na Scottsdale, na kote kuyapitia yale mabonde kule. Kisha tunao Mkutano mkuu wa Wafanyabiashara Wakristo unaotokea kule, ambao ni mkutano mkuu wa siku tano mwishoni mwa mikutano hii yote. Wamepanga kwamba ningeweza kuyazungumzia madhehebu yote, kila moja ya makanisa yao kotekote kwenye eneo zima la mji mkuu wa Bonde la Maricopa katika Phoenix. Nao wataanza kwenye tarehe kumi na tano. Kwa hiyo nitaondoka hapa yapata siku kumi mapema, kusudi . . . Nitasimama labda kumwona rafiki yangu mwema, Ndugu Moore, na baadhi yao nikishuka. Ndipo kutakuwa na theluji kote kwenye mapito hayo, na kadhalika, na kwenda katika wakati. Halafu mimi . . . wengi wenu ninyi watu ni wahudumu.

8 Naye Ndugu Roy Borders, ikiwa yupo hapa asubuhi ya leo, yeye kwa kawaida huiweka mikutano katika utaratibu wanapoitisha mikutano. Ndipo kwenye likizo hizi za Krismasi, vema, kwa kawaida mimi hufanya ratiba ya mahali nitakapoenda mwaka unaofuata, lakini mwaka huu kwa namna fulani nilijisikia kutokufanya hivyo. Ninajisikia kwamba nitaenda na kufanya mkutano mmoja, na halafu mahali Yeye anaponiongoza kwenye mkutano unaofuata nitaenda kutoka hapo. Halafu kutoka kwenye mkutano unaofuata, popote pale, niende tu jinsi Yeye anavyoniongoza.

9 Nami ninatazamia sasa jambo fulani litukie mnamo mwaka huu. Na maono mengi yamekuwa yakinijia hivi majuzi. Hivi majuzi asubuhi lingine kubwa tena na lote likihusu na kuonekana kama kitu fulani kikuu kinakaribia kutukia. Kwa hiyo ninaendelea tu kumtumainia Yeye. Baadhi yake hata siyaelewi. Wala hatuyaelewi maono, zaidi sana ni kama mifano wala hatuyapati kikamilifu wakati mwingine, lakini tunajua kwamba ni ya kweli, haidhuru. Kwa hiyo, yatatimia. Ninayaandika.

10 Na kwa hiyo ninaamini imetangazwa pia, ama inapaswa kutangazwa, kwamba halmashauri ya wadhamini na halmashauri ya mashemasi pia watakutana hapa maskanini katika umoja, mkutano wa pamoja, saa moja kesho usiku. Sasa hebu nitangaze hilo tena kusudi kama mashemasi,

popote walipo, kama wako kwenye chumba hicho kingine wanaweza kusikia kwenye ile maikrofoni ndogo, kwamba kesho usiku kwenye saa moja, wote mchungaji—wote mchungaji, halmashauri ya mashemasi na wadhamini pia, ndio kwanza niambiwe dakika chache zilizopita kwamba walikuwa wakutane kesho usiku. Naye Ndugu Neville anataka kuiona halmashauri yake ya mashemasi na kuzungumza nao, nao wadhamini wanao wakati wao wa kawaida wa kukutana, na kwa hiyo watakutana pamoja kesho usiku.

11 Sasa, asubuhi ya leo, kabla hatujalikaribia Neno, sasa, loo, hebu tusiwe na haraka kuhusu chochote. Mnayo siku nzima leo, na usiku wa leo na kesho, hebu tuchukue tu wakati wetu wa—wala tusiyaharakishe mambo haya. Hakika, ninajua watu huwa wachovu ama huchoka na, au, wanataka kwenda nyumbani, mwajua, kwa ajili ya ninii yao. . .kuharakisha, wana chakula chao cha kutwa, nao waume zao wanakingojea. Mbona, basi, hilo—hilo ni sawa, toka tu polepole. Na—na—na wengine wenu mnaotaka kukaa, sawa. Nasi hatuninii. . .Sio lazima kufanya kazi kesho, sasa, na kwa hiyo tuuchukue tu muda wetu. Na hiyo ndiyo sababu niliwazia badala ya kuhubiri tu kwa saa tatu ama nne, ningechukua saa nane ama kumi katika mafundisho. Mnaona? [Ndugu Branham na kusanyiko wanacheka—Mh.]

12 Watu hao wote kutoka Georgia na Alabama walinifanya kujisikia vizuri sana hivi majuzi usiku. Ninaamini nilikuwa huko nje karibu na ofisi, na wote walikuwa wameondoka ila Billy, naye akasema. . .Ndugu West na hao wengine, ambao ni marafiki wazuri na waaminifu sana, siwaoni hapa, bali ninadhani wako hapa, walipiga simu na kusema, "Vema, hivi Ndugu Branham atakuwa na Shule ya Jumapili, Jumapili asubuhi?" Basi kulikuwa kukiganda kwa baridi huko Louisville, habari zilisema wanafunga barabara kuu ndani na nje, na barabara zinateleza.

13 Billy alisema, "Vema, kuna uwezekano," kasema, "yeye hushuka kule." Kasema, "Labda Ndugu Neville ama yeye, mmoja wao."

14 Kasema, "Vema, uwezekano huo ni mzuri kutosha, sisi hapa tunakuja!" Kotekote kutoka huko chini Alabama, na kwenye barabara zinazoteleza, na mimi—mimi sistahili kuwa na marafiki kama hao. Sasa, hiyo ni kweli. Si—sistahili kuwa na marafiki kama hao. Kuna jambo fulani kulihusu. Nami ninachukia sana kuutangaza huo mkutano, nikijua ya kwamba ninao watu wanaoamini Ujumbe, nao—nao wanakuja, na—nao wananipenda.

15 Na mimi—mimi sikuzote nimetamani kupendwa. Nilipokuwa mvulana mdogo sikupendwa na mtu yeyote. Hakuna mtu aliyekuwa na haja na mimi. Nilikuwa hapa Indiana, nilizaliwa Kentucky, kwa hiyo nilikuwa mtafuna mahindi kwa

hawa watoto huku. Katika familia, wavulana wote, karibu wote, walivuta sigara na kunywa pombe na kila kitu, ila mimi. Nami nilikuwa—nilikuwa mtu anayeepukwa katika familia, na anayeepukwa shuleni, na kazini nilikuwa anayeepukwa, na kila mahali nilipoenda nilikuwa ni wa kuepukwa. Ndipo hatimaye nilipompata Mtu aliyenipenda kweli, Yesu, na Yeye alisema, "Nitakupa baba na mama, ndugu, dada, na marafiki."

16 Ndipo basi jambo la ajabu ni vile majaliwa Yake makuu ya hekima, ya jinsi Yeye hufanya kazi katika ninii Yake, nje. Inaonekana kana kwamba upendo huo una hisia ya ajabu ndani yake; si hisia, bali m—mjibizo. Ndipo basi ninaangalia huko nje miongoni mwa watu, kwa kuwa Yeye ameniita kuwa mtumishi Wake, nami ninaangalia huko nje miongoni mwa watu na kuona dhambi ikiingia kisiri, ndipo inanibidi tu kuirarua mle ndani kwa yote yaliyo ndani yangu, mnaona, kuirarua. Basi hiyo inaifanya ionekane ni ngumu kwa. . .kwa njia yangu ya kuiangalia, mbona, kuyasema mambo hayo. Lakini, hata hivyo, kule chini kabisa, upendo wa kweli hufanya hivyo. Mnaona, upendo wa kweli.

17 Sasa, kama mvulana wako mdogo ama msichana mdogo alikuwa akicheza barabarani ambako magari yanapita mbio, nawe ulijua muda si muda wataumia. Sasa, kama akisema, "Mbona, Papa, ninataka kuwa hapa nje," hivi ungesema, "Nautakia heri maskini moyo wako, Kadogoo, wewe endelea tu moja kwa moja na kucheza barabarani"? Huyo si baba halisi. Ikiwa itakulazimu kumvuta upesi maskini jamaa huyo na kumpa kichapo, kumkemea, kumfunga, chochote kingine, kumwondoa kwenye barabara hiyo, atauawa. Hiyo ni kweli? Vema, hivyo ndivyo huna budi kufanya na Injili. Inakubidi kutikisa na kusukuma, na—na—na kujaribu kufanya kila uwezacho kuwalainisha watu. Sasa, natumaini kila mtu analifahamu hilo jinsi hiyo. Ni—ninatumaini tu kwamba siku moja hapa baada ya yote kwisha na halafu wakati taji zitakapoondolewa kutoka usoni mwetu, tutafahamu basi.

18 Ndugu Way, mimi. . .ile Biblia nzuri ambayo wewe na Dada Way mlinipa kama zawadi ya Krismasi, hiyo itakuwa tu ni kitu kizuri cha kuandikia muhtasari wangu badala ya kitabu kama hiki, ninapopata nafasi ya kuyapiga chapa. Sitaki kuandika, maana siwezi kusoma maandishi yangu mwenyewe, basi mtu yeyote mwingine atayasomaje? Niliwaambia nilikuwa na hati mkato yangu mwenyewe. Nami inanibidi kuichunguza mwenyewe nione yale nimesema. Basi ni—nitaichapisha siku moja. Ni Biblia yenye karatasi zisizounganishwa, ambapo unaweza tu kuchukua kama hapa. Ninayo mafungu mawili hapa asubuhi ya leo, mahali pawili ninapotaka kusoma. Na katika Biblia hii aliyonipa, unaichomoa namna *hii,* nawe unaweza kuchukua karatasi moja kutoka Mwanzo, Ufunuo, mahali popote, na kuviweka vyote pamoja, na kuvisoma moja kwa

moja namna hiyo, mnaona. Halafu mahali padogo hapa nyuma upande wa nyuma penye karatasi isiyounganishwa, unaweza tu kuzirejea moja kwa moja, kwenye Maandiko yote yaliyoandikwa kwenye ujumbe huo na kadhalika. Ni nzuri sana. Kwa hiyo natumaini nitasaidia kuleta nafsi nyingi kwa Kristo nayo.

19 Mungu ambariki kila mmoja wenu. Ninataka kusema tena kwa ajili ya zawadi nzuri za Krismasi ambazo kila mmoja alinipa. Kanisa lilinipa suti mpya, loo, jinsi ninavyoithamini! Kisha nikapata suti mbili mpya za Krismasi. Ndugu yangu, lile kanisa dogo huko Macon, Georgia, huko chini, Ndugu Palmer, lilinitumia suti mpya. Nayo maskani ikanipa suti mpya, na kuna vitu vingi vizuri nilivyopewa, na—na zawadi za Krismasi kwa njia ya fedha. Ambazo, idara ya kodi ya mapato inaniambia ya kwamba kama ni zawadi ya Krismasi na imeandikwa "Zawadi ya Krismasi" ama "Zawadi ya Siku ya Kuzaliwa," chochote kile, unaweza kuikubali; la sivyo kwamba inanibidi kuninii. . . ina—inaingia kazini, ambalo ni sawa. Na hakika ninamshukuru kila mmoja wenu, mimi pamoja na mke wangu, na watoto, basi sisi sote tunatoa shukrani zetu kwa kila mmoja, kila mmoja wenu, mu wazuri sana. Tunatamani tungeweza kurudi na kumpa kila mmoja wenu zawadi, bali kamwe huwezi kufanya hivyo, mwajua, unaninii tu. . . Jamani, ni—nisingeweza kufanya hivyo. Laiti ningaliweza, bali kamwe si—siwezi. Nina hakika mnaelewa. Nami najua hiyo ndiyo hisia ya ndugu yangu mpendwa anayeketi hapa, pia. Tunajisikia tu watu wanatupenda jinsi hiyo, tunawathamini.

20 Sasa, hebu tuviinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi, na tuwe tayari, tupate kuuanza Ujumbe asubuhi hii.

Mbele za Mungu aliye hai tunakuja sasa, watulivu, na katika kumcha Yeye, tunakuja katika Jina la Bwana Yesu, tukijua ya kwamba tusingeweza kuja na kusema, "Sasa, Baba, huyu hapa William Branham, ama, Orman Neville," ama yeyote tuwezaye kuwa, tungekataliwa upesi. Bali tunalo hakikisho ya kwamba Yeye alisema, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, litajaliwa." Kwa hiyo sidhani ningeweza kupata, nikitumia jina langu, chochote kutoka Kwake. Lakini ninajua wakati nikilitumia Jina la Mwana Wake, basi ninapata haja yangu, kwa kuwa Yeye ndiye ninayemtumainia. Ndiye tunayeishi Kwake na kuwa na uhai wetu. Nasi tunashukuru asubuhi ya leo, Mungu, kwa ajili ya yote Yeye anayomaanisha kwetu, na hayo ndiyo maisha yetu makamilifu na utu wetu.

21 Ninakushukuru Wewe kwa ajili ya kanisa hili dogo, kwa ajili ya mchungaji wake, na kwa ajili ya wadhamini na mashemasi, washiriki wote. Pia ninashukuru kwa ajili ya Roho Mtakatifu ambaye huwachunga. Jalia huyo Roho Mtakatifu mkuu aendelee kuwaongoza na kuwaelekeza kwenye mapito ambayo Yeye angewataka wapitie. Nikisoma kwenye Maagano, la Kale na lile Jipya, na pia katika *Wakati wa Nikea*, na jinsi ambavyo

wakati maradhi yalipopiga miongoni mwa watakatifu, kanisa lote lilikusanyika pamoja, kwa moyo mmoja wakamwita Mungu, nayo maombi yao yakajibiwa. Kila mmoja wao kama washiriki wa Mwili wa Kristo, wakifunga na kuomba, naye Mungu akasikia na kuyajibu maombi. Baba, jalia kanisa hili dogo lifungwe sana katika vifungo vya upendo mmoja kwa mwingine na Roho Mtakatifu, hata litakuwa kama mmoja wa hao, hata hakutakuwako na msuguano wowote miongoni mwetu katika mwaka huu ujao. Jalia kuwe tu na upendo mkuu wa kitauwa, na kila mtu akitembea katika njia ya Kristo, hata wasafiri wengi waliochoka njiani watakuja na kuokolewa. Jalia isemwe ya kwamba utakapoingia milango ya jengo hili dogo, ya kwamba Uwepo wa Mungu utakutana nawe pamoja na makaribisho matamu. Ondolea mbali maradhi miongoni mwetu, Bwana.

22 Nasi tunashukuru kwamba tunayo mioyo yenye njaa kulisikia Neno Lako. Endelea kuipa mioyo yetu njaa kwa ajili Yako, Bwana. Kama vile Daudi wa kale alivyosema, "Kama ayala aoneavyo shauku kijito cha maji, nafsi yangu inakuonea kiu." Nikiwazia juu ya maskini ayala, kulungu kama tungemwita siku hizi, ambaye ameraruliwa na mbwa mwitu, na anatokwa na damu. Anayapoteza maisha yake, naye hana budi kupata maji endapo anatarajia kuishi. Mara anapopata maji, uhai wake unafanywa upya. Jalia tuwe na kiu hivyo, Bwana, kwamba hatuna budi kumpata Kristo kama tutaishi, hatuna budi kuwa na Kristo kama tutakuwa Kanisa tunaloomba. Kama tukiishi maisha tunayotaka kuishi, hatuna budi kuwa na Kristo ama tufe.

23 Sasa wakati tukilifungua Neno Lako asubuhi ya leo, kupata faraja na mawe ya kukanyagia, kutuleta karibu na Yeye, ninaomba, Baba, ya kwamba Roho Mtakatifu atatufungulia sisi Neno, kwamba sisi, Bwana, kama watumishi Wako, tutahamasishwa vizuri zaidi kuukabili mwaka mpya. Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

24 Sasa, ninawazia asubuhi ya leo ya kwamba juu ya msingi wa kuwa ni mwaka mpya, nilifikiri lingekuwa ni jambo jema labda kwamba niweke kando Ujumbe wangu wa Mwaka Mpya mpaka usiku wa leo, nirudi hapa katika baadhi ya Maandiko ya shule ya Jumapili, na nichukue fungu la kuzungumzia kwa kitambo kidogo, juu ya moja la masomo muhimu sana niyajuayo katika Biblia. Ni Fundisho ambalo Bwana wetu alihubiri kwanza, Fundisho la kwanza ambalo Yesu alihubiri, nami nadhani ingekuwa vema kulifanya fundisho letu la kwanza la mwaka.

25 Sasa, ni baridi kwa yeyote wenu, inua mkono wako, mwasikia baridi kidogo? Nilidhani niliisikia hapa juu. Doc, popote ulipo, kwa namna fulani fungulia tanuru kidogo tu, kwa sababu ninaisikia hapa ikienea. Najua hapana shaka mnaisikia hapo nje, baadhi yenu watu, hasa sana mlio na watoto.

26 Sasa hebu tufungue katika Biblia zetu asubuhi ya leo, kwenye Waefeso, mlango wa 4 wa Waefeso, na hebu tuanze kusoma kwenye cha 11, kifungu cha 11 cha Waefeso mlango wa 4. Halafu tutafungua basi kutoka hapo, kuanzia hapo, hadi kwenye Yohana 3:1-12, na kusoma mahali pawili katika Maandiko. Tukisoma sasa kutoka kwenye mlango wa 4 wa Waefeso, na kifungu cha 11, kuanzia:

> *Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii;. . . wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu;*
>
> *Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma* itendeke, *hata mwili wa Kristo ujengwe:*
>
> *Hata na sisi sote* tutakapofikia. . . *umoja wa imani, na kumfahamu sana Mwana wa Mungu, hata kuwa mkamilifu . . . mtu mkamilifu, hata kufika kwenye cheo cha kimo cha utimilifu wa Kristo:*
>
> *Ili tusiwe tena watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa elimu, kwa hila ya watu, na ujanja, ambapo wanangojea kudanganya;*
>
> *Lakini tuishike kweli katika upendo na kukua hata* tumfikie *yeye katika yote, yeye aliye kichwa, Kristo:*
>
> Kwa kuwa *katika yeye mwili wote ukiungamanishwa na* umeshikamanishwa *kwa msaada wa kila kiungo, kwa kadiri ya utendaji wa kila sehemu moja moja, huukuza mwili upate kujijenga wenyewe katika upendo.*

27 Sasa, nimesoma hayo kusudi yawape kitu fulani cha kuendelea kusoma mkiisha kufika nyumbani. Sasa nitasoma fungu langu kutoka kwa Yohana 3, Andiko linalojulikana sana:

> Ndipo *palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo, mkuu wa Wayahudi:*
>
> *Huyo alimjia Yesu usiku, akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu, umetoka kwa Mungu: kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye.*
>
> *Yesu akajibu, akamwambia, Amin, amin, nakwambia, Mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.*
>
> *Nikodemo akamwambia, Awezaje mtu kuzaliwa, akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?*
>
> *Yesu* akijibu. . . *akajibu, Amin, amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa . . . Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu.*

*Kilichozaliwa kwa. . .mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa. . .Roho ni roho.*

*Usistaajabu kwa kuwa* nakwambia, Ninyi *hamna budi kuzaliwa mara ya pili.*

*Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini* huwezi *kujua unakotoka* wala *unakokwenda: kadhalika hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.*

*Nikodemo* akasema. . .*akajibu, akamwambia, Yawezaje kuwa mambo haya?*

*Yesu akajibu, akamwambia, Je, wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya huyafahamu?*

*Amin, amin, nakuambia kwamba,* Lile *tulijualo twalinena, na* lile *tuliloliona twalishuhudia; wala ushuhuda wetu* hamwukubali.

*Ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, wala* ninyi *hamsadiki, mtasadiki wapi niwaambiapo. . .mambo ya mbinguni?*

28 Sasa, Mungu alibariki Neno Lake. Nami ninataka kuchukua somo asubuhi ya leo la Fundisho la kwanza la Yesu. Fundisho la kwanza la Yesu, lilikuwa: *Huna Budi Kuzaliwa Mara Ya Pili.* Hilo lilikuwa ndilo Fundisho Lake la kwanza. Sasa, kwa njia ya shule ya Jumapili, kusudi nisihubiri na kujipweleza sauti usiku wa leo, nimewazia moyoni mwangu ya kwamba hili ni jambo ambalo linaonekana ni fumbo, na kwa watu, tunasikia mengi sana kulihusu wakati wote, nami niliwazia lingekuwa ni jambo zuri asubuhi ya leo kama tukilichambua somo hili kikamilifu, tulitatue. Na hilo ndilo la kwanza kabisa: *Huna Budi Kuzaliwa Mara Ya Pili.* Nalo ni la kilindi sana.

29 Na sisi—sisi tunaona ya kwamba kuna maana nyingi sana mbalimbali ambazo watu huweka kwake. Karibu makanisa yote yanasema ya kwamba huna budi kuzaliwa mara ya pili, lakini kila moja lina tafsiri zao—zao tofauti kwa jambo hilo, kile kuzaliwa mara ya pili kunachomaanisha. Huenda nikaenda kwa kanisa la Methodisti asubuhi ya leo, waseme, "Tunaamini ya kwamba huna budi kuzaliwa mara ya pili." Mnalifasirije? Niende kwa kanisa la Baptisti, "Nasi tunaamini ni lazima uzaliwe mara ya pili." Mnalifasiri namna gani? Nami ningeenda kwa kila kanisa, nasi tungekuta, kama tungalienda kwa madhehebu yote mbalimbali mia tisa ya makanisa, kungekuwako na fasiri mia tisa mbalimbali. Kwa hiyo, kwa kuwa kunazo tafsiri nyingi mbalimbali, na hata hivyo Fundisho la Biblia, hapana budi kuwepo, na kunayo, Kweli mahali fulani.

30 Kwa hiyo, sasa kumbukeni, halikusema, "*Unapaswa* kuzaliwa mara ya pili," bali "*huna budi*!" Sasa, sisi, kama watu wanaozungumza Kiingereza, tunaelewa vile neno *huna budi* linavyomaanisha, hilo ni, "bila shaka, huna budi kulifanya."

Mnaona, ni *lazima*! Sio "inakupasa kufanya, ingekuwa afadhali kama ungelifanya," bali "*huna budi* kuzaliwa mara ya pili!" Loo, laiti tungalilichukua tu Neno hilo asubuhi ya leo na kulifafanua, linavyomaanisha, jinsi ambavyo haiwezekani kabisa . . . Na halafu kama ni muhimu hivyo na ni kuu hivyo, kwamba haiwezekani kabisa kuingia katika Ufalme wa Mbinguni, wala hata kuuona, mpaka umezaliwa mara ya pili, na tafsiri nyingi sana mbalimbali za neno hilo, *kuzaliwa mara ya pili,* inatupasa kukutafuta kwa moyo wetu wote, tujue maana yake.

31 Hakuna mtu aliyepo humu ndani ambaye anataka kwenda katika mateso, hakuna mtu. Na ninyi hamwendeshi maelfu ya maili, kwenye barabara zilizojaa barafu, na kutumia riziki yenu, fedha zenu, kuja tu kanisani hapa ili, vema, tuseme, kupeana mikono na watu (ingawa mnapenda kufanya hivyo), na kunisikia mimi na mchungaji na wahudumu wengine tukilihubiri Neno (mnapata hilo popote mlipo, wachungaji, wahudumu, kama tu tulivyo sisi, watumishi wa Kristo), bali kuna kitu kinachowavuta hapa, na mahali hapa hasa. Kwa hiyo, ni jukumu letu sisi kama wachungaji, kuona ya kwamba kundi hili linalishwa, na kulishwa vyema, kwa sababu Mungu Mwenyezi atahitaji damu yenu mikononi mwetu. Kwenye siku ya Hukumu, tutawajibika kwa ajili yenu. Kwa hiyo, tukiona wajibu huu mkuu sana uliowekwa juu yetu, naye Mungu ametupa watu ambao wanatupenda na wanaokuja kutusikiliza, basi inatupasa kutumia wakati wetu sikuzote tukiziangalia nafsi zenu. Na wakati kitu kidogo cha kwanza tunachokiona kikiibuka ambacho si sahihi, ni jukumu letu kumjia mtu huyo, kwa sababu sisi ni wachungaji tunaowachunga kondoo hao. Na kama nikimwona kondoo huyo akila gugu litakalomuua, afadhali nimfukuze kutoka kwenye gugu hilo; niling'oe gugu hilo mara moja kutoka kwake asije akalifikia, kwa sababu litamuua huyo kondoo.

32 Basi kuna gugu linalojulikana katika nchi za Magharibi ambalo ninii, mnyama anaweza kulila, linaitwa "gugusumu." Sijui kama mtu yeyote alipata kulisikia ama la, gugusumu. Naam. Farasi anaweza kulila hilo, na huwezi kufanya lolote naye. Anakuwa tu mkaidi. Huwezi kuweka tandiko juu yake, wala huwezi kufanya lolote naye. Linaitwa "gugusumu." Nawe huna budi kuwaweka mifugo yako—yako mbali na gugu hilo. Basi kama itamfanya farasi kula kitu fulani, iwapo farasi, hasa, atakula kitu kinachomtupilia kwenye hali hii, katika kifafa, mbona, ungekuwa mchungaji duni sana kumwacha farasi wako ale gugu, gugusumu. Inaonyesha kwamba wewe hujali.

33 Naye mchungaji halisi, mtumishi halisi wa Kristo atakuwa ni mfano duni wa Kristo, kumwona kondoo akila kitu mbacho kitamwondoa, ama kumfanya mkaidi mbele za Mungu, mvunjaji wa Neno Lake, mvunjaji wa amri Zake. Hupaswi kufanya hivyo. Inakupasa kuangalia hilo kwa makini sana.

34 Kwa hiyo Fundisho hili kuu la Yesu Kristo ambalo limeandikwa hapa mbele zetu, katika Biblia, "Hamna budi kuzaliwa mara ya pili." Kunazo tafsiri zake nyingi sana mbalimbali, kama nilivyosema hapo kabla, mpaka, niliwazia asubuhi ya leo, kwa ajili ya wengi ambao wamekuwa wakiniuliza ilivyomaanisha na jinsi wangeweza kuwa Mkristo halisi, ndipo niliwazia labda tungelikaribia tu hili somo na kulichukua dhahiri tu kadiri nijuavyo jinsi ya kuwapa ninyi. Nalo si katika njia ya mahubiri, ni kwa njia ya kufundisha shule ya Jumapili, watu waweze kuupata Ujumbe. Sasa, tafsiri nyingi za "kuzaliwa mara ya pili."

35 Na sasa ninasema jambo hili, nami ninajua linaingia kwenye kanda, nami ninataka kusema jambo hili kwa wachungaji ambao labda wataipokea kanda hii. Nadhani labda ni tofauti kidogo tu na vile kanisa la kawaida linavyolifundisha, ninafundisha na kuamini, na ninaamini ninaweza kulithibitisha vya kutosha kwa Maandiko, ya kwamba unazaliwa kwa Roho kisha unabatizwa katika ule Mwili kwa Roho Mtakatifu.

36 Sasa, wengi wao wanafundisha ya kwamba unakuja tu na kutambulishwa mbele ya kusanyiko, na kadhalika, kama mwe—mwenye dhambi, ya kwamba unataka kumkubali Kristo kama Mwokozi wako binafsi, ya kwamba huko ndiko Kuzaliwa upya. Wengi wanaamini ya kwamba ubatizo wa maji ndio Kuzaliwa upya. Na baadhi yao wanaamini kwamba una—unazaliwa kwa maji unapobatizwa katika maji. Na kuna tafsiri zake nyingi sana mbalimbali. Wengi wao, wengi wanaamini ya kwamba kukariri kanuni ya imani na kuamini fundisho la kanisa, kukubali tu na kusema, "Ninaamini katika kanisa takatifu la *Fulani-na-fulani*. Na—nami ninaamini Mungu kuwa Mwo—Mwokozi wa mwanadamu, na kadhalika. Basi tangu siku hii na kuendelea, ni—ninakuwa mfuasi wa kanisa hili, na ushirika pamoja na Wakristo." Wao wanaamini ya kwamba huko ndiko "kuzaliwa mara ya pili."

37 Na ingawa kanuni ya imani wanayokariri, siamini ya kwamba tungeweza kuikosoa, baadhi yazo ni safi na takatifu, baadhi yazo ni za Kimaandiko sana, bali Maandiko hayo hayatumiwi mahali panapofaa. Na, hata kuyatumia Maandiko, ninaamini ya kwamba Kuzaliwa upya ni kitu fulani zaidi ya hayo. Haidhuru unalimaanisha vizuri jinsi gani, ninaamini kitu fulani kwamba Kuzaliwa upya ni zaidi ya makusudi yako mema na mawazo yako, nia, kumepita hayo.

38 Sitaki kusema jambo hili kukufuru, wala silikashifu dhehebu lolote la kanisa, bali mengi yake hunikumbusha juu ya—juu ya—Myahudi fulani, ninii kidogo. . .ni utani. Nami siamini ya kwamba utani unapaswa kutolewa mimbarani, si mahali pa mizaha. Na kwa hiyo kuleta tamshi hili nililo nalo niani mwangu, sio kwa ajili ya utani, bali kuonyesha dhihirisho la yale ninayomaanisha. Kwamba kasisi Mkatoliki

wakati mmoja alienda nyumbani pamoja na . . . Ijumaa, pamoja na mwongofu mpya wa kanisa Katoliki. Basi mwongofu huyo Mkatoliki alikuwa ameoka hemu, naye akasema, "Padre, samahani, baada ya kumbukumbu yangu kunijia, hii ni Ijumaa. Lakini ninaamini kwamba kulingana na fundisho letu kuu la kanisa, ya kwamba wakati mmoja nilikuwa Myahudi, nawe ukaninyunyizia maji matakatifu ukanigeuza kutoka Myahudi nikawa Mkatoliki. Sasa nitanyunyizia maji yayo hayo kidogo juu ya hemu hii na kufanya samaki kutoka kwake." Sasa, hilo, kusema hivyo hakuifanyi samaki. Ingali ni hemu, haidhuru hayo maji yangejifanya matakatifu jinsi gani.

39 Basi haidhuru ni jinsi gani tunavyojaribu kufikiri tuko sahihi katika kukariri kanuni ya imani ama kujiunga na kanisa, ungali vile ulivyokuwa mpaka utakapozaliwa kweli mara ya pili kwa Roho wa Mungu. Haikubadilishi. Kanuni yako ya imani, kujiunga na kanisa, au kubadilisha mawazo yako, ama makusudi yako mazuri, ingawa huenda yakaonekana ni mazuri, yangali si sahihi. Kuna jambo fulani halina budi kutukia, kuzaliwa upya ni tukio, jambo fulani linalotukia. Kwa hiyo si hilo linalosababisha kuzaliwa upya. Sasa, makanisa mbalimbali, yangesema, "Vema, wewe kubali *hili* ama uamini *lile,* nalo ni sawa." Bali sio sawa.

40 Sasa, kwanza kabisa, kulirejesha kwenye msingi, sababu hatuna budi kuzaliwa mara ya pili ni kwa kuwa Biblia inatufundisha ya kwamba sisi "sote tulizaliwa katika dhambi, tukaumbika katika uovu, tukaja katika ulimwengu huu tukisema uongo." Basi hiyo inatuonyesha ya kwamba asili yetu, kwanza kabisa, ni yenye dhambi kwa kuanzia. Sisi hatuna uzuri wowote, kwanza kabisa. Kwa hiyo hatuwezi kudai chochote kwa werevu wetu, unyofu wetu, *wala* jinsi tulivyo wakuu, ama jinsi tulivyo wadogo, ama chochote zaidi, sisi kwa jumla tumekosea, kwa kuanzia. Wala hakuna kitu hata kidogo tunachoweza kufanya juu yake. Huwezi . . . Yesu alisema, "Ni nani, kwa kuwazia, anayeweza kuongeza ki- . . . kimoja kwenye kimo chake, kipimo kimoja kwenye kimo chake?" Unaweza kuyachukua mawazo yote, uote ndoto zote, ulisome, ulitafiti, ulichunguze, na kila kitu kingine, wala huwezi kujisaidia hata nukta moja. Kwa hiyo hiyo inayatupilia yote nje. Ninashukuru sana inafanya hivyo, kwa kuwa kama lilitegemea wazo la kujua jambo fulani, la werevu, maskini sisi watu tusio na elimu tungeachwa nje, kwa hiyo tusingekuwa na nafasi. Lakini Mungu alibadilisha hilo, ama hakuwa nalo jinsi hiyo hapo mwanzo. Makanisa sikuzote hulifanya gumu. Mungu hulifanya rahisi. Kwa hiyo imefikia mahali ambapo sisi sote tunaweza kuona, sisi sote tunaweza kulipata. Ni kwa yeyote atakaye.

41 Sasa, sasa, mtu mmoja asingeweza kumwokoa mwingine. Sasa, haileti tofauti yoyote yale mtu yeyote anayojaribu kusema, hakuna mtu anayeweza kumwokoa mwingine. Haidhuru ni mwerevu jinsi gani, ofisi yake ni ipi, acha awe mchungaji,

kasisi, askofu, kadinali, ama papa, hawezi kuwa na jambo moja kuhusu kuyaokoa maisha ya mwanadamu yeyote, kwa sababu yeye mwenyewe ni mwenye dhambi, aliyezaliwa katika dhambi, akaumbika katika uovu, akaja ulimwenguni akisema uongo. Yeye ni mwongo kwa kuanzia, na neno lolote ambalo angeweza kusema lingekuwa ni uongo kama lilikuwa ni kinyume na Neno la Mungu na mpango wa Mungu.

42 Lakini Mungu alifanya mpango kwa ajili ya mwanadamu kuokolewa. Naye mwanadamu hawezi kuongeza lolote kwenye mpango huo. Ni mpango wa Mungu. Na huo ndio mpango tulio nao, tunaotaka kuchunguza asubuhi ya leo. Mpango wa Mungu ni upi? Yeye alisema, "Neno la kila mwanadamu liwe uongo, Langu liwe Kweli." Kwa hiyo, hatutathubutu kubadilisha sentensi moja, kulifanya kitu kingine. Haidhuru ni jinsi gani taratibu zetu za ibada na kadhalika zinavyosomeka, inatupasa kuzisahau hizo. Hili ni Neno la Mungu. Kamwe haliwezi kufanywa kwa njia nyingine yoyote. Mungu anao mpango, Yeye amefanya mpango.

43 Pia, kumbukeni, jambo la kwanza, mpaka utakapozaliwa mara ya pili kamwe hutaelewa. Mara mbili Yeye alilinena. "Mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuingia katika ule Ufalme." "Mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi hata kuuona huo Ufalme." Sasa, hilo limewekewa vituo, pia. Neno, katika kuyafanya maneno hayo yote, wananiambia kwamba iliwabidi kuyaandika yote, hao, ndipo waliposema, "amin, amin," huko ni kuyatenga maneno, kama vile he—he—herufi kubwa. "Amin, amin, nawaambia!" Nalo hilo neno katika mahali pamoja, ama mahali pengi, limetafsiriwa "kabisa." "Kabisa, kabisa, nawaambia!" Ni nani aliyesema hayo, ni kadinali, kasisi, mchungaji, mwinjilisti, papa? Mungu Mwenyewe! Sasa, hakuna udhuru. Hataweza kabisa, hataweza kabisa, hawezi kwa njia nyingine yoyote, haidhuru yeye ni mkuu jinsi gani, kwamba jina lake ni gani, jinsi alivyo mkubwa, ama jinsi alivyo maarufu, hawezi hata kuufahamu Ufalme wa Mungu mpaka azaliwe mara ya pili. Ni somo kubwa. "Amin, amin, nawaambia!" Angalieni. Nenda kachukue tafsiri ya Kiyunani, utaona, sio *kuona* kwa "macho" yako, *unaona* kwa "moyo" wako. Unaona, huwezi kuuona Ufalme wa Mungu kwa macho yako, kwa sababu ni Ufalme wa kiroho. Mnaona? Kwa maneno mengine, "Kamwe hutaweza kuelewa Ufalme wa Mungu mpaka utakapozaliwa mara ya pili." Yote ni siri iliyofunuliwa. Basi wakati unapozaliwa mara ya pili, mipango ya Ufalme, Ufalme Wenyewe, unakuwa ni halisi kwako.

44 Kama vile kondrakta kulijenga jengo, isipokuwa angeweza kuisoma ramani yake hamna haja ya yeye kujaribu kujenga jengo, endapo haielewi ramani yake. Halafu basi anapoielewa ramani, basi anajua jinsi ya kulijenga hilo jengo. Hivyo—hivyo ndivyo ilivyo. Hilo ndilo linalotendeka kuhusu kuujenga Ufalme

wa Mungu. Huna budi kuielewa ile Ramani, na hutaijua Ramani mpaka umezaliwa mara ya pili. Basi unapozaliwa mara ya pili na halafu unaikanusha ile Ramani, ni kitu gani kinachotukia?

45 Msichana mdogo wa kupendeza ambaye hivi majuzi... Nilikuwa nikiambatana na mama yake tulipokuwa wadogo. Naye alikuwa ni mwanamke wa kupendeza, mzuri. Jina lake ni Huff sasa, jina lake lilikuwa Lee kabla hajaolewa. Nilipokuwa nikilichunga Kanisa la Baptisti la Milltown, wao walikuwa ni wafuasi wa Kanisa la Ndugu wa Muungano, lakini, loo, walinipenda vizuri sana. Naye...Nilikuwa nikiambatana naye. Waliishi huko nyuma kabisa nyuma ya kwa Ndugu Wright hapa. Kuninii...Nami nilikuwa nikienda nyumbani mwao, naye maskini msichana huyo alikuwa ni msichana mdogo mzuri sana, naye alikuwa ni maskini rafiki yangu wa kike. Basi Ndugu Lee, mtu mzuri, mwaminifu kwa kanisa, maoni ya Ndugu wa Muungano kuhusu kanisa, basi usiku mmoja yeye alinialika kwenda nyumbani pamoja naye na kukesha usiku kucha. Nami nikasema, "Ndugu Marrion, nita—nitafurahia kufanya hivyo." Na kwa hiyo baada ya ibada kwisha, vema, mimi na hu—huyo msichana tuliingia kwenye gari na tukaenda. Nami ilinibidi kufungua malango dazani moja, ninaamini, tukipitia ubavuni mwa kilima, na kupanda juu, kuifikia nyumba kubwa mno ya magogo. Vema, tuliketi nje barazani tukawangojea mama na baba yake, na dada yake mdogo, waje. Walipokuja, sote tuliingia ndani na kula chakula kidogo cha mchana usiku huo. Mama alikuwa ametoa vitu nje nasi tukala, na—na mimi na huyo baba tulikuwa tukilala pamoja kwenye orofa ya chini, kwenye kitanda kikubwa mno cha manyoya, na—na majani makavu chini yake, mwajua, malazi mazuri kweli. Ni mazuri zaidi kuliko yoyote ya maskini magodoro haya ya Beautyrest mliyo nayo, nawaambia hivyo. Na kwa hiyo sisi...Mama na hao wasichana wawili wakapanda kwenye orofa ya juu.

46 Basi usiku huo tulipokuwa tumelala mle, Ndugu Lee aliota ndoto. Naye alikuwa sikuzote amejadiliana nami kuhusu ubatizo wa maji katika Jina la Bwana Yesu Kristo. Hakuuamini. Naye alikuwa ni kondrakta. Kwa hiyo alisema, "Ndugu Branham, ndio kwanza niote ndoto." Kisha akasema, "Niliota nilienda huko New Albany. Nami nilikuwa nikijenga nyumba ya mtu fulani, naye akanipa ramani yake. Bali nilipoona njia fulani ambayo alikata madirisha yake na kuweka mahali fulani, nilisema 'Hilo si sahihi. Kamwe haliwezi kuwa ni sawa. Hilo ni kinyume. Hilo, hilo si sawa.' Kwa hiyo nikalijenga jinsi nilivyodhania ilikuwa sahihi. Basi aliporudi kutoka Florida, kutoka kwenye likizo yake, nilikuwa karibu nimeimaliza nyumba yake.

47 "Aliiangalia hiyo nyumba, naye akaenda na kuichukua ramani yake na kuiangalia hiyo, kisha kasema, 'Aisee, umeijenga nyumba yangu vibaya!'

"Nami nikamwambia, 'La, sijaijenga nyumba yako vibaya.'

"'Vipi kuhusu mahali *fulani-fulani*?'

"'Vema,' akasema, 'hapo hasa si mahali pake.'

48 "Akasema, 'Ibomoe! Kama unatarajia nikulipe, utaijenga jinsi ramani ilivyosema.'"

49 Naye akasema, "Unafikiri nini juu ya hilo, Ndugu Branham?"

50 Nikasema, "Kuna kijito kinachotiririka papa hapa chini ya nyumba hii hapa." Nasi tukakiendea.

Akasema, "Sitaki kubomolewa kokote kwenye siku hiyo."

51 Nikasema, "Ipate vizuri, sasa. Ijenge kulingana na ramani!"

52 Jinsi lilivyolipia, hivi majuzi tu mmoja wa nanii wake. . .Kisha msichana wake akaolewa na mvulana mzuri, mwamamume mzuri. Yeye ni mtengeneza mashine huku kwenye viwanda vya mitumbwi, naye mvulana huyo alikuwa amekatwa vidole vyake *namna hii*, mtu mzuri. Nao wana familia nzuri, wasichana watatu wadogo, na mmoja wao ni. . . wote Wakristo, nao wanaimba wakiwa watatu. Kama tukiwa na mkutano hapa wanakuja kutuimbia. Basi mmoja wa hao wasichana wadogo alisomea utaalamu wa muziki wa piano, naye alikuwa ni mwalimu wa muziki mwororo wakati alipokuwa ni mtoto tu, miaka kumi na mitano, kumi na sita. Ndipo watoto shuleni wakaanza kumchokoza kuhusu mambo mbalimbali, na kwa kuwa Mkristo, nalo likamtia wasiwasi na kumfanya achanganyikiwe, naye akarukwa na akili. Basi walimpeleka Louisville, nao walikuwa wampeleke kwenye hospitali ya wendawazimu Jumatatu iliyofuata. Wala wasingeninii, hao madaktari wasingeniruhsu kumwona. Basi nikaenda kule kama mgeni na kuketi kando ya kitanda pamoja na baba na mamake. Ndipo wakati nilipokuwa nimeketi pale, Roho Mtakatifu akaingia kwenye, hii, Nyumba ya Wagonjwa ya Mama Yetu wa Amani huko Louisville, mahali wanapowapeleka wagonjwa wenye wasiwasi, wakati kungali kuna matumaini kwao. Halafu, wasipoweza kuwafanyia lolote, wanawapeleka Madison, Indiana. Basi msichana huyo alikuwa akipelekwa Madison juma hilo, wao. . .alikuwa hawezi kusaidika. Huku tumeketi pale, ono likatokea mbele yetu, likazungumza na msichana huyo katika Jina la Bwana Yesu. Ndipo mama akanishika ghafla gotini, akanyosha mkono akamshika mumewe mkono, na kusema, "Kamwe halikosei!"

53 Nikasema, "Kamwe msijali, atakuwa sawa." Nikaondoka humo jengoni upesi.

54 Usiku huo kwenye saa tatu, simu ikalia, ama ninaamini ilikuwa kidogo kabla ya saa tatu, kabla sijaja kanisani usiku huo. Ilikuwa ni Jumapili. Naye baba, huku moyo wake umechangamka sana, akasema, "Nisingeweza kwenda nyumbani, nikishikilia hizi habari njema, Ndugu Branham."

Akasema, “Daktari aliingia na kumchunguza msichana wangu. Akasema, ‘Imekuwaje kwake? Anaweza kwenda nyumbani kesho.’” Wakati mama alipokuwa amelala maiti majuma machache yaliyopita, hapo hao watatu walikuwa kule chini, maskini msichana huyo akiwa mzuri alivyoweza kuwa, yeye na rafiki yake wa kiume, vizuri. Loo, nawaambia, ile Ramani! Neno la Mungu Ndilo la kuelezea ratiba ya jinsi inavyotupasa kuzaliwa mara ya pili.

55 Kwanza, tunajihesabu wenye dhambi na wanaostahili kuhukumiwa. Nasi sote tumezaliwa katika dhambi na tukaumbika katika uovu, hakuna sehemu yetu iliyo nzuri. Nia zetu ni mbaya, nafsi yetu imepotoka, mawazo yetu kila mara ni maovu, kila fikra ya kimawazo ya nia ya mwanadamu ni mbaya, mwenye dhambi, na pia kwamba mwili wetu ni dhaifu, roho yetu si nzuri, nasi tumejaa upotovu. Basi kitu kimoja cha upotovu kingewezaje kuleta kitu kingine kizuri kutoka kilicho kiovu? Hebu niseme hivi, kwamba katika Ayubu, mlango wa 14, yeye alisema, “Kwa kuwa mwanadamu aliyezaliwa na mwanamke, amejaa huzuni na shida, hata hivyo huchipuka kama ua, ananyauka.” Na kuendelea, kama nabii anavyoendelea kuzungumza, yeye alisema, “Ni nani anayeweza kuleta kitu safi kutoka kwa kilicho kichafu? Hayupo hata mmoja!” Ukishusha ndoo yako katika kisima na kuvuta ndoo ya maji, nayo yametuama, yananuka; unaangalia ndani yake, nayo yamejaa matope, na wadudu wadogo wamo kwenye maji hayo, hakuna njia kamwe ya kuirudisha ndoo yako na kupata ndoo safi. Hicho kisima chote kimechafuka. Nayo nafsi yote, nia na mwili wa mwanadamu umechafuliwa na dhambi. Yeye amezaliwa katika dhambi, kimwili, akaumbika katika uovu, kisha akaja ulimwenguni akisema uongo, hivi kwamba nafsi yake mwenyewe imechafuka. Hakuna kitu kizuri! Mmoja hawezi kumkomboa mwenzake, kwa kuwa yote ni makosa. Nawe huwezi kuchukua ndoo nzima ya maji hapa, ambayo yamechafuka, na ndoo nyingine ambayo imechafuka, na kuyachanganya pamoja, una uchafu zaidi. Hakuna utakaso kwake.

56 Lakini Mungu alidhamiria kumwokoa mwanadamu. “Aliweka juu Yake uovu wetu sote.” Adhabu ya—ya dhambi, wakati ambapo unazaliwa katika adhabu ya dhambi, ni mauti. Dhambi ni mauti. Nayo adhabu ilikuwa kubwa sana hata hakuna mmoja wetu angaliweza kumsaidia mwenziwe, kwa hiyo ilibidi pawe na Mtu Ambaye angeweza kuilipia adhabu hiyo.

57 Vipi kama, asubuhi ya leo, adhabu ya kuondoka humu chumbani ilikuwa ni dola bilioni mia moja? Hakuna hata mmoja wetu angaliweza kuondoka, maana hakuna mmoja wetu mwenye thamani hiyo. Lakini basi kama mtu akija aliyekuwa na za kutosha kutulipia sisi sote!

58 Inahitaji Mmoja. Hatuwezi kulifanya. Ilichukua Mmoja

Ambaye alistahili. Loo, jinsi ninavyotamani ningesimama hapa kwa muda kidogo, na kurudi nyuma niwachukue Ruthu na Naomi, na kuonyesha jinsi ambavyo mkombozi wa jamii, kuikomboa mali iliyopotea, ilibidi awe, kwanza, anayestahili, ilibidi awe wa jamaa wa karibu. Kwa hiyo, Mungu, Roho, Yehova, akafanyika Jamaa yetu, kwa kuchukua mfano wa mwili. Akawa Jamaa wa karibu. Ilibidi awe hivyo. Kisha ilibidi Yeye awe anastahili. Na Yeye Ndiye aliyeitoa ile Chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli. Yeye Ndiye Ambaye aliyachukua maovu yetu.

59 Mfano wa kupendeza nilio nao hapa katika Hesabu. Ninayo Maandiko yangu yaliyoandikwa hapa chini. Katika Hesabu, ule mfano wake mzuri uko mle ndani, ni, loo, kwa jumla ni wa kupendeza sana kama mngeweza kuuona, ni ile nyoka ya shaba iliyoinuliwa juu nyikani. Jinsi ambavyo Israeli, nyoka huyo kwao alikuwa ni muumo wa mauti, wala hapakuwapo na tiba. Hapakuwapo na tabibu miongoni mwao ambaye alikuwa na tiba wala dawa. Walikuwa na matabibu miongoni mwao, bali sio kwa ajili ya huo muumo. Kama tu vile nimesema, hakuna matabibu miongoni mwetu wanaoweza kutibu dhambi. Ni muumo wa mauti, nasi sote tuna hatia, sote tumeumbika katika uovu. Sisi sote tuna hatia. Lakini Mungu alifanya nini? Walikuwa na hatia basi, kisha mauti yalipaswa kulipwa, adhabu ya mauti. Lakini Mungu alimwagiza Musa kuisimamisha wima nyoka ya shaba, na kuiweka kwenye nguzo, kwamba hakuna kitu watu wangaliweza kufanya, hakuna pesa walizopaswa kulipa, hakuna kitu hata kidogo, hakuna kanuni za imani walizopaswa kukariri, hakuna makanisa waliyopaswa kujiunga nayo, ni "tazama tu uishi." Mnaona jinsi ilivyo rahisi? Tazama uishi! Usijiunge na kanisa, hakuna mhemko, haikubidi kupata hisia ya ajabu. Tazama tu uishi! Hivyo tu. Rahisi sana. Sio, "Kama unaweza kukumbuka Amri zote Kumi, utaishi." Sio, "Kama unajua maagizo yote." Ni, "Tazama tu uishi." Hivyo tu ndivyo ulivyopaswa kufanya. Na kila mtu aliyemwangalia Yeye aliishi.

60 Yesu, wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, akizungumza na Nikodemo hapa, Yeye alisema, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa." Vivyo hivyo hana budi! Kwa nini? Kwa njia ile ile, kwa jambo lile lile, kwa kusudi lile lile, kufanya kazi ile ile. Mara nyingi hili huwakanganya watu wanapomwona nyoka akimwakilisha Yesu. Huyo nyoka alimwakilisha Yesu, kiasi hiki, hivi mliona huyo nyoka alikuwa amekufa? Hapakuwapo na uhai ndani yake. Yesu alikufa. Kama vile Kaini, hapo alipomwua Habili, Habili alikufa madhabahuni pamoja na dhabihu yake; baada ya Habili kutoa dhabihu yake na kuichinja dhabihu yake kwa ajili ya dhambi yake, ndipo akafa kwenye madhabahu yale yale pamoja na dhabihu yake. Ili upate kuzaliwa mara ya pili, inakubidi kufa kwenye madhabahu

pamoja na Dhabihu yako, mfu tu kama Yeye alivyokuwa. Nawe umezaliwa mara ya pili. Nyoka hakuwa na uhai ndani yake.

61 Nawe unasema, "Kwa nini ilikuwa ni shaba?" Shaba inawakilisha hukumu, hukumu ya Kiungu. Hivi uliona katika Biblia, katika Agano la Kale, madhabahu yalifanyizwa kwa shaba, ambapo dhabihu iliteketezewa? Shaba inazungumzia hukumu. Kama vile Eliya, katika siku zake, alienda kuziangalia anga, aone kama mvua yoyote ilikuwa inakuja baada ya maombi yake, naye akasema, "Anga zinaonekana kama shaba." Ilikuwa ni nini? Hukumu ya kiungu juu ya watu wasioamini, taifa lisiloamini ambalo lilikuwa limemwacha Mungu. Ilikuwa ni Hukumu ya Kiungu, shaba! Naye nyoka mwenyewe, umbo lake liliwakilisha dhambi iliyohukumiwa tayari, kwa kuwa nyoka alihukumiwa katika bustani ya Edeni. Naye alikuwa, nyoka, aliyehukumiwa.

62 Nasi tunapomwangalia Kristo, unaona ile adhabu. Yule pekee, Mungu Mwenyewe, aliyefanyika mwili. Mungu akija duniani, na kujitwika dhambi yetu sote, nayo hukumu na hasira ya Mwenyezi Mungu ilimwagwa juu ya mwili Wake, na hapo ukapasuliwa msalabani. Hiyo ndiyo hukumu halisi. Yeye alikanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya Mungu, peke yake. Peke yake, Yeye alitembea barabarani. Peke yake, Yeye alikufa pasipo na msaada kutoka kwa Malaika, kutoka kwa mwanadamu, kutoka kwa Kanisa Lake, kutoka kwa mama Yake, kutoka kwa ndugu Zake, kutoka kwa Baba Yake; ameachwa na Mungu, wanadamu na maumbile. Alikufa, peke yake, apate kutuonyesha ya kwamba hata maumbile yenyewe hayawezi kutusaidia katika saa ya mauti. Hakuna rafiki, hakuna kasisi, hakuna papa, hakuna mchungaji. Ni mauti. Lakini kulikuwako na Mtu Ambaye aliichukua kwa ajili yetu.

63 Hapakuwapo na uhai ndani ya yule nyoka. Alikuwa kabisa amekaushwa. Hiyo ilikuwa ndiyo adhabu. Yeye alikufa hata n—nchi ikajionea aibu. Alikufa hata nyota zikaona aibu. Aliteseka hata jua lisingeweza kuangaza. Aliteseka hata mwezi ukazima taa zake. Aliteseka mpaka hata elementi za dunia zikawa nyeusi sana na zenye giza hata ikawa ni usiku wa manane, giza sana hata ungaliweza kuligusa. Hapakuwa na kitu. Hakuna mtu aliyepata kuteseka namna hiyo ama angeweza kuteseka jinsi hiyo, hakuna mwanadamu angaliweza kupitia hayo. Lakini Yeye aliyapitia hayo. Mungu aliweka juu Yake uovu wetu sote, na kuweka hukumu Zake juu Yake, na Yeye akakanyaga shinikizo la mvinyo ya ghadhabu ya Mungu, pekee, pasipo na msaada. Hapakuwapo na kitu cha kumsaidia. Mungu aliiweka adhabu. Kila kitu kilikuwa chini ya adhabu hiyo, wala hakuna kitu kingaliweza kumsaidia, maana sisi sote tuna hatia. Hakuna kuhani mkuu angaliweza kuja kumsaidia. Hakuna kitu kingaliweza kumsaidia, hakuna papa, hakuna Malaika. Kila kitu kilisimama nyuma na kuliangalia. Hayo yalikuwa ndiyo

majira makuu kuliko yote yaliyowahi kuwapo katika historia ya ulimwengu. Alikufa mpaka hapakuwapo na tone moja la uhai lililosalia ndani Yake, akawa kama yule nyoka wa shaba, pambo tu lililokaushwa limening'inia msalabani.

64 Sasa, njia ya kuendea kuzaliwa huku, kuna njia ya kukuendea. Na kukukaribia kuzaliwa huku, inakubidi kupitia hatua fulani. Ni kama tu vile chochote kilicho hai, chochote kinachoishi tena, hakina budi kufa kwanza. Wala huwezi kudumisha roho yako ile ile. Huwezi kudumisha tabia zako zile zile. Huwezi kudumisha mawazo yako yale yale. Huna budi kufa. Huna budi kufa kama Yeye alivyokufa! Huna budi kufa madhabahuni Pake, kama Habili alivyofanya na mwana-kondoo wake. Huna budi kufa pamoja na Mwana-kondoo wako. Huna budi kufa. Kufia mawazo yako mwenyewe, upate kuzaliwa kwenye mawazo Yake, kuacha nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yako. Huna budi kuyawaza mawazo Yake. Na sasa, ndugu, dada, hebu niseme hili kwa akili kadiri nijuavyo kulisema. Unawezaje kuyawaza mawazo Yake kisha ulikane Neno Lake, na hata hivyo udai umezaliwa mara ya pili? Hebu jiulize tu swali hilo. Unawezaje? Huwezi. Kama umezaliwa mara ya pili, unayo mawazo Yake. Endapo nia ya Kristo iko ndani yako, basi wewe ni kiumbe kipya. Biblia inafundisha hilo. Na kama ndugu yeyote angetaka, vema, unaona hilo *kiumbe,* angalia hilo neno *kiumbe* katika ka—kamusi ya Msamiati, nawe utaona ya kwamba neno *kiumbe* hapo limefasiriwa ama kutafsiriwa, "kiumbe kipya," kwa sababu wewe ni kiumbe kimoja, mwanadamu aliyezaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili hapa duniani, na sasa wewe ni kiumbe kipya kilichozaliwa kwa Roho. Mawazo yako mwenyewe yamekufa. Yamekufa sana hata yamekaushwa kama yule nyoka wa shaba, ama kama vile Yeye alivyokufa wakati mbingu na nchi na kila kitu kilishuhudia Yeye alikuwa amekufa.

65 Yeye alikufa mpaka akawa amekufa sana hata Damu Yake na maji vikatengana mwilini Mwake. Mauti Yake yalikuwa ni makuu sana hata, nasema, u—ulimwengu ukashikwa na wazimu. Ukatetemeka, ukatikisika hata miamba ikaanguka kutoka milimani. Ni kitu gani kingaliweza kufa namna hiyo? Hakuna papa akifa angeweza kufanya hivyo, hakuna mchungaji akifa angeweza kufanya hivyo. Lakini wakati Mungu, katika mwili, alipokufa msalabani, ulimwengu uliingia wazimu, kujua ya kwamba Neno lenyewe la Mungu lililonenwa, miamba na mavumbi, marungu na miti iliyoning'inia ardhini, na nyota na mwezi, Neno Lake hasa lililonenwa lilimwona Muumba wao akifanyika mwili, na dhambi ikimwagwa juu Yake. Ghadhabu ya Mungu ilimwagwa juu Yake hata mwezi ukazima nuru yake, jua likazima nuru yake, dunia ilikuwa na mtetemeko wa wasiwasi, kuingia wazimu. Ungalipasuka vipandevipande kama kusingalikuwa na siku za usoni kwa ajili yetu, kila kitu.

66 Na kama elementi Zake za ardhini, zilipoangalia, zikaona

yale yaliyokuwa yakitukia, zilitikisika zikafikia hali hiyo, inapaswa kunifanyia nini mimi na wewe? Nafsi zetu zinapaswa kufanya nini tunapoangalia na kuona yale Mungu aliyotufanyia? Nayo yote yalikuwa ni kwa ajili yako wewe na mimi. Inapaswa kutufanyia nini? Kuendelea katika dhambi? Mungu aepushe. Lakini kuepukana na dhambi, na kufia dhambi. Hivi hamwoni yale dhambi iliyomfanyia Yeye? Dhambi ilimwua. Naye alichukua adhabu ya dhambi, ili aweze kuleta haki ya Mungu kwako na kwangu. Kwa hiyo wakati haki ya Mungu inapotujia, dhambi imekufa katika utu wetu unaopatikana na mauti. Loo, ninatumaini mnaliona.

67 Naam, kuzaliwa mara ya pili huna budi kupitia hatua ya mauti, kila kitu hufanya hivyo. Hebu chukua punje ya mhindi, kama hindi hilo linatarajia kuishi tena, halina budi kufa kwanza. Kama punje ya ngano ikitarajia kuishi tena, haiwezekani kabisa. . .Kwa kuwa, hindi hilo, ngano hiyo, ua hilo, mti huo, unyasi huo, mboga hizo, kila kitu kinachotarajia kuishi tena hakina budi kufa kwanza. Basi utaliepukaje? Huna budi kufa kwanza. Huna budi kufa. Ufe namna gani? Kwa nafsi yako, ufie kila kitu, kusudi upate kuzaliwa tena. Huna budi kufanya hivyo. Usipokufa, kamwe huwezi kuishi tena.

68 Pia, angalieni, hivi ulijua kila siku kitu fulani hakina budi kufa ili uweze kuishi? Sasa kwenu nyinyi Waadventista Wasabato mlio miongoni mwetu, watu wengi husema, "Nisingemwua kuchakulo, Ndugu Branham. Nisingemwua kulungu au sungura, samaki, maana siamini ya kwamba inatupasa kuua vitu." Ndugu yangu, hivi ulijua ya kwamba mboga na kadhalika unazokula ni uhai pia? Huna budi kuziua. Na njia pekee ambayo unaweza kuishi katika maisha haya, kitu fulani hakina budi kufa upate kuishi kwa uhai wake uliokufa. Sasa, kama inabidi kitu fulani kife upate kuishi kwa maisha yake yapatikanayo na mauti hapa duniani, kuishi kibinadamu, hivi Kitu fulani haikubidi kufa ili kwamba kwa Uzima Wake wewe uweze kuishi Milele? Jiulize tu swali hilo. Nacho Hicho kilikuwa ni Kristo, maana hakuna mwingine asiyepatikana na mauti. Mwana pekee ndiye asiyepatikana na mauti. Na Yeye anajitolea Mwenyewe kwako kwa kumkubali Yeye tu. Sasa, hakina budi kufa.

69 Sasa, hiyo haimaanishi kufungua ukurasa mpya sasa, mwaka huu mpya. Unasema, "Ndugu Branham, nimekuwa nikija hapa kwa muda mrefu. Nimekuwa mshiriki wa kanisa. Mwaka huu Mpya nitafungua ukurasa mpya na kuanza upya." Hilo halimaanishi hivyo. Sio "kufungua ukurasa mpya," bali hakika kufa na kuzaliwa mara ya pili. Unaona? Huna budi kujisikia mwenye hatia sana unaposimama Mbele Zake, kama unapitia njia ya Methodisti ama njia ya Baptisti, ama njia yoyote unayopitia, huna budi kuwa na hatia sana na kujisikia mwenye hatia sana mpaka wewe. . .Itakuua. Hiyo ni kweli.

Ita—itakuua. Maisha yako ya kilimwengu yatakufa papo hapo. Inakupasa kujihesabu mwenye hatia sana Mbele za Mungu mpaka maisha yako ya kilimwengu yanakufia pale pale. Swa—swali la dhambi limekwisha kwako wakati unaposimama Mbele Zake. Unapoangalia namna hiyo, una hakika kuishi, kwa sababu unakufa. Na jinsi pekee unavyoweza kuishi tena ni kuwa . . . kufa kwanza upate kuishi tena.

70 Sasa mnaona ninayoendea, sivyo? Aa-ha. Kuzaliwa kupya kulivyo, kule kuzaliwa upya. Kwanza, kufa, upate kuzaliwa mara ya pili. Basi kama ungali una mambo ya ulimwengu ndani yako, hujazaliwa mara ya pili. Nawe utadai vipi umezaliwa mara ya pili na ungali una mambo ya ulimwengu yamening'inia juu yako? Unaona? Unawezaje kufanya hivyo?

71 Mkristo mchanga hivi majuzi, kundi la watu . . . Sisemi sivyo walivyo. Bali katika kuangalia baadhi ya picha, wanawake Wakristo, wanaume Wakristo, wote wa kupendeza, wamechanganyikana, wamevaa nguo za kuogelea, katika kuogelea. Mnaona? Ni ninii tu . . . Wao walisema, "Huo ni upendo halisi." Huo ni uchafu halisi! Sio upendo. Upendo huonyeshwa tofauti na hivyo.

72 Nafsi zetu zimewekwa kwa imani kwenye madhabahu Yake ya shaba, hukumu ya Mungu, na sadaka yetu inateketezwa. Sasa kumbukeni, wakati Eliya, chini ya hizo mbingu za shaba, alipoiweka dhabihu ya Mungu juu ya madhabahu, hiyo dhabihu iliteketezwa. Baali asingeweza kuiteketeza dhabihu yake. Sitaki kusema hili, bali sina budi kulisema. Basi unapoenda kanisani na kukubali kanuni zao za imani na aina zao za mabatizo, na sadaka unayokusudiwa kuiweka mwenyewe mle, huenda ukasimama ukitetemeka, kunena kwa lugha, kukimbia kote sakafuni, ama huenda ukaamka ukilia, lakini, kama sadaka hiyo imepokelewa na Mungu, imeteketezwa; ulimwengu umekufa kwako. Umekwisha, kwa kuwa tunajihesabu wenyewe tumekufa na kuzikwa. Tumekufa na tuna . . . Tumefichwa katika Kristo. Tumefichwa ndani ya Kristo! Na, mbali na hayo, ndipo—ndipo tukiisha kufa na kuzikwa na kufichwa katika Kristo, basi tunatiwa muhuri kwa Roho Mtakatifu.

73 Mnaona yale ninayomaanisha sasa? Umekufa. Nafsi zetu zimewekwa juu ya hukumu Yake ya Kiungu. Hiyo ni shaba. Wakati nafsi zetu zimewekwa juu ya madhabahu ya hukumu ya Kiungu, adhabu ilikuwa ni nini? Mauti. Basi unapojilaza kwenye madhabahu ya Mungu, ambayo yametangaza mauti juu ya mwenye dhambi, unawezaje kusimama kutoka hapo, ukiwa hai katika dhambi, iwapo Mungu aliikubali hiyo dhabihu? Hiyo ni wazi sasa? Unakufa! Kweli unateketezwa, nawe umegeuzwa kuwa jiwe. Hakuna kitu kilichoachwa kwako ila umbo hili unalosimama ndani yake, kama yule nyoka wa shaba, kama Kristo alivyokuwa wakati walipomtoa msalabani akiwa mfu na baridi. Umekufa! Kwa sababu gani? Uko kwenye madhabahu

ya Mungu ya hukumu. Hukumu Yake ni nini? Wakati Hakimu ametoa hukumu Yake, hukumu ya adhabu Yake ni nini? Mauti. Nawe unapoiweka nafsi yako juu ya madhabahu Yake ya hukumu, ni mauti kwako. Sasa mnalipata?

74 Loo, huenda ukaamka kutoka hapo na kufanya lolote, huenda ukacheza katika Roho, huenda ukalia kama—kama mtu yeyote angelia, huenda ukakimbia huku na huku sakafuni, huenda ukajiunga na kila kanisa, huenda ukafanya lolote utakalo, (ninawazungumzia Wapentekoste sasa), kisha urudi moja kwa moja na kumnajisi mke wa mtu, uivunje nyumba ya mtu, baadhi yenu wanawake. Utarudi moja kwa moja haidhuru Neno linakujia wewe mara ngapi ufanye mema na kadhalika, hutalitambua Hilo. Kamwe hamtaziacha nywele zenu zikue, enyi wanawake, ama hilo. Kamwe hamtavalia sawasawa. Ungali utakuwa kama ulimwengu hasa, kwa sababu hujaufia ulimwengu bado, ungali hai nao.

75 Baadhi yenu wanaume hamtaacha kunywa pombe, kuvuta sigara. Hamtaacha kuwatamani wanawake wachafu waliovalia kizinifu, mnapowaona mtaani, badala ya kugeuza mgongo wako, uondoke. Ungali utaendelea kutamani vivyo hivyo tu. Kwa sababu gani? Ungali hai pamoja na ulimwengu bado. Lakini wakati dhabihu hiyo imepokelewa, wewe umekufa. Hiyo ni kweli. Mnasikia ninayomaanisha? Mnaelewa ninayozungumzia?

76 Sasa, nafsi yako imewekwa juu ya yale madhabahu ya hukumu ya Mungu ya shaba, ndipo Mungu anaipokea dha-. . .Sasa, inaonyesha ya kwamba hujaipokea bado, ikifanya hivyo. . .Kama—kama ungali hai ulimwenguni, Mungu kamwe hajaichukua. Sasa, ninyi watu mnaozungumza kuhusu kumpokea Roho Mtakatifu na jinsi inavyowapasa kungojea muda mrefu, haya basi. Mpaka Mungu atakapoipokea dhabihu hiyo, mpaka itakapowekwa juu ya hukumu Zake kule, mpaka hukumu Zake zitakapoziua hisi zako kweli! Huenda ukasema, "Vema, nitafungua ukurasa mpya." Hivyo sivyo. "Vema, ninajua nilikuwa nikivuta sigara, nitaacha kuvuta sigara." Hilo bado silo. Mpaka Mungu atakapoipokea dhabihu hiyo kwenye madhabahu Yake ya shaba, madhabahu Yake ni hukumu. Hukumu Yake ni nini? Mauti. Hiyo ndiyo adhabu.

77 "Nafsi inayotenda dhambi," inabaki humo, "itakufa." Sijali yale umefanya.

78 Yesu alisema, "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, na kusema, 'Bwana, si nimefanya *hili* na kufanya *lile*?' Yeye aseme, 'Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao uovu.'" Mnaona?

79 Wakati dhabihu hiyo inapopokelewa na moto, nao unapanda juu namna *hiyo*, nao moshi unapanda juu, unainuka pamoja na dhabihu yako ukaingia mbinguni, nawe umetiwa muhuri kutoka kwa mambo ya ulimwengu basi. Nafsi yetu iko madhabahuni Mwake.

80 Umefanya nini basi, ukiisha kufa, basi inakupasa kufanya nini? Ndipo unachukuliwa mimba upya. Unachukuliwa mimba upya. Ulichukuliwa mimba kwanza katika uovu. Sasa umechukuliwa mimba katika kitu fulani kipya. Ni kitu gani? Neno lililo hai. Amina. Loo, hilo linalibadilisha sasa, sivyo? Sasa, tumemalizana na masumbuko, ukiisha kuona yale unayopaswa kufanya. Sasa ni jambo gani linalotukia? Umezaliwa upya, katika Neno lililo hai. Ni kitu gani? Neno linakuwa hai ndani yako. Unaanza kuona mambo vinginevyo. Ambapo wakati mmoja usingeweza kuona hilo, sasa unaliona. Kuna kitu fulani tofauti sasa. Kinayafanya Maandiko yote yaje pamoja. Yanafanya kila kitu kushikamana vizuri kabisa. Halafu, sasa—sasa kitu fulani kimeanza kutukia. Sasa, unayafia mawazo yako mwenyewe, sasa umechukuliwa mimba, kwa kuwa tumesafishwa na maji ya Neno. Hiyo ni kweli?

81 Unafanyaje na mtoto mchanga mara anapozaliwa? Kumwosha. Hiyo ni kweli? Na mara mtu amekufa kwa nafsi yake, amezaliwa na Mungu, anaoshwa kwa maji ya Neno. Amina. Kama linasema, "Jina la Yesu," unasema, "Jina la Yesu"; likisema, "Huna budi kuzaliwa mara ya pili," wewe unasema jambo lile lile. Lolote Mungu asemalo, wewe umeoshwa kwa maji ya Neno. Amina.

82 Sasa, uko tayari sasa kwa maisha. Uko tayari kuwa ninii…kuanza sasa. Sasa umezaliwa upya, umezaliwa katika familia ya Mungu, ukiwa na mzazi mpya. Naam, bwana. Walimu wako walikuwa…Sasa unao walimu waliopo sasa, una Mzazi mpya. Huwezi kuzaliwa bila mzazi. Kwa hiyo kama umezaliwa katika udugu wa kanisa, hayo ndiyo uliyo nayo. Iwapo umezaliwa katika kanuni ya imani, haya basi. Lakini kama umezaliwa katika Mungu, ukachukuliwa mimba katika Neno Lake, una Mzazi Mpya, huyo ni Mungu, tayari kukujulisha Neno Lake miongoni, pamoja nawe, kulinena Hilo kupitia kwako. Loo, Mzazi mpya, Mzazi huyo ni Mungu. Yeye yuko tayari kulichukua Neno Lake sasa ambalo amelinena tayari, na kuliweka Hilo ndani yako na kulifanya hai. Mnaona? Sasa unayo mafunzo yako sasa. Uko tayari, uko tayari kuingia katika mafunzo sasa, mafunzo ya mtoto. Hiyo ndiyo sehemu iliyo ngumu, wakati unapowazia unapaswa kufanya jambo *hili,* nalo Neno linakukatakata na kukuonyesha jambo lingine. "Mbona, wanaamini hilo huku…" Hilo halileti tofauti yoyote yale wanayoamini. Haya hapa yale Mungu aliyosema! Huna budi kuwa kwenye kazi ya Baba. Sasa unazaliwa mara ya pili. Sasa unawekwa sawa, unanyoshwa. Unaye Mzazi mpya.

83 Kwa hiyo, kama umezaliwa mara ya pili na unaye Mzazi mpya, basi una asili mpya. Asili ya kale imekufa, nawe una asili mpya. Wakati mmoja ulikuwa ukielekea njia moja, sasa unaelekea njia nyingine. Wakati mmoja ulikuwa ukienda *hivi*, chini, sasa unaenda *hivi*, juu. Upendo wako uko kwenye mambo

yaliyo juu. Upendo mpya! Huyapendi mambo ya ulimwenguni tena, upendo wako ni wa Mungu. Hujali yale mwanadamu asemayo, jinsi wanavyokucheka na kusema wewe ni "mtindo wa kale," ama chochote kilicho namna hiyo, hujali, kwa sababu umezaliwa kutoka juu na upendo wako umewekwa—umewekwa kwenye mambo yaliyo juu. Mungu hakuonei aibu wala wewe humwonei aibu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo wewe ni . . . Soma mlango wa 11 wa Waebrania papa hapa. Nimeiandika. Ni kwa nini tu, jinsi, watu katika siku hizo, jinsi walivyofanya. Jinsi ambavyo walizunguka-zunguka wakivaa ngozi za kondoo, jangwani, na wahitaji, na kila kitu kingine, ambao ulimwengu haukustahili kuwa nao. Mnaona? Isomeni, itawafaa. Nanyi mwaweza kuona pale, vile watu wakati asili yao imebadilishwa, yale yanayotukia.

84 Sasa, "Una asili ya namna gani basi, Ndugu Branham?" Asili Yake. Kama ningalikuwa na asili ya baba yangu, basi ningefanya mambo baba yangu aliyofanya. Lakini sasa kwa kuwa nimezaliwa mara ya pili, inategemea baba yangu alikuwa ni nani. Kama umezaliwa tu kanisani, unaye baba wa kanisa, nawe unaweza kumwita "baba" ukitaka. Unaweza kumwita chochote unachotaka, kwa sababu yeye ni baba yako. Lakini kama Baba yako ni Mungu, nawe umezaliwa katika familia ya Mungu, unayatafuta mambo yanayohusiana na Mungu. Hiyo ni kweli. Basi wewe ni mwana wa Mungu. Asili yako ni asili ya Mungu. Ndipo wakati baadhi yao, loo, unawasikia, wengine wanasema, "Loo, kanisa letu linaamini ya kwamba siku za miujiza zimepita." Ungewezaje kuamini siku za miujiza zimepita wakati ile asili yenyewe ya Mungu iko ndani yako? Wakati Yeye kwa jumla ni mwujiza? Asili yake ni mwujiza, tabia Yake ni mwujiza, utu Wake wote ni mwujiza. Unawezaje kuwa kitu kingine chochote ila mwujiza? Kuzaliwa kwako upya ni mwujiza. Maisha yako mapya ni mwujiza. Hata asili yako ni mwujiza. Jinsi unavyoweza kuangalia nyuma na kusema, "Hayo mambo yamekufa. *Hili* ni kweli." Mnaona? Wewe ni kiumbe kipya, kiumbe kipya. Hakika.

85 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Ndipo wakati watoto wachanga walipozaliwa wote walikuwa ni vifaranga wa kuku ila mmoja. Yeye alikuwa ni tai. Alikuwa jamaa mdogo wa kipekee. Kwa jumla alikuwa ni tofauti, lakini, mnaona, alizaliwa katika jamii nyingine. Mbe—mbe—mbegu na yai zilikuwa ni tofauti, zilifanya ndege tofauti. Hakika alionekana si wa kawaida, alitenda kigeni kwa hao wengine, bali alikuwa—alikuwa akitenda tu kiasili, kwa sababu asingeweza kufanya cha zaidi, maana yeye—yeye alikuwa ni tai. A—asili yake ilikuwa ni tai, kwa hiyo hayo tu ndiyo angaliweza kuwa ilikuwa ni tai. Bali kuna wengi sana wao nje katika madhehebu haya, hao kweli ni tai, bali haionekani sawa kuwaona wakigaagaa katika matope na kadhalika ya ulimwengu. Mnaona? Hilo ni kusema, hao ni

jukumu letu, kuwatafuta.

86 Siku moja maskini mama tai alikuja huko, basi unafikiri kuku huyo angeweza kumweka ardhini tena? Haijalishi alitoa mlio kiasi gani, vizuri jinsi gani, alivyosema, “Njoo hapa, kipenzi. Nimepata kitu papa hapa, njoo.” Loo, jamani! Upendo wake ulikuwa kwenye mambo yaliyo juu, naye akaenda kukutana nayo. Hakuna madhehebu tena kwake. Hawawezi kumwita atoke Kwake.

87 Naye mtu aliyezaliwa na Mungu, huwezi kumwita arudi katika uchafu huo wa dhambi uliooza tena. Yeye amekufa, na amezaliwa mara ya pili. Yeye ni kiumbe kipya. Yeye yuna tabia ya Tai. Hana budi kuingia angani na kupaa. Hana budi kupaa huko juu aliko Mama yake, Mzazi wake.

88 Na hivyo ndivyo wewe. . .mtu anayeamini, anavyojaribiwa, “Loo, njoo kajiunge na kanisa letu. Sasa, huo ni ulokole. Si—si—siku. . .”

89 Sasa, kama maskini tai huyo huenda amesimama huko nje naye akamsikia mama huyo akilia, naye akaangalia huku na huku na kusema, “Huko ni wapi?” Hapa, labda yeye alilia kitu kama hiki kwa maskini tai huyo mdogo, “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.”

90 Naye huyo mama akasema, “Siku za miujiza zimepita, chwi, chwi, chwi, chwi. Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama hicho! Huo ni ulokole!” Loo, jamani!

91 Mbona, usingeweza kumshikilia tena. Ninaweza tu kumsikia akisema, “Mama, nitafikaje huko juu?”

92 “Pigapiga tu mabawa yako, kipenzi. Hivyo tu ndivyo unavyopaswa kufanya. Wewe ni tai. Tembea tu kwa imani.”

“Itakuwaje, Mama?”

93 “Sijui. Endelea tu kutembea.” Huyu hapa anakuja. Kupigapiga kwake mara chache za kwanza, aliketi kwenye nguzo ya ua. Alifika juu hivyo, haidhuru. Akasema, “Njoo tu, nitakushika.” Jambo ndilo hilo.

94 Asili mpya, utu upya, uumbaji mpya, tabia ya Baba yako. Nawe unaamini na unapenda kila Neno ambalo Yeye alisema. Kila Neno la mwanadamu ni uongo, kinyume na Neno hili. Hili ni Neno la Mungu. Mnaona? Biblia ni ya kweli. Sijali yale kanisa lisemayo, Biblia ingali ni ya kweli, kwako, maana asili yako imebadilishwa. Sasa, kama una ba—baba wa kanisa, utamwamini huyo baba wa kanisa. Lakini iwapo una Baba Mungu, utaliamini Neno la Mungu. Kama unaye baba kanisani, utaamini hilo kwa sababu wewe ni wa asili yake, huyo ni baba yako. Lakini iwapo Baba yako ni Mungu, basi utaliamini Neno la Mungu. Kama wewe ni kanisa, uta—utaliamini neno lake, utaliamini neno la kanisa, utakuwa vile kanisa lisemavyo. Lakini ikiwa umezaliwa mara ya pili, basi utaamini yale Mungu

asemayo, maana Mungu ndiye Baba yako; sio ulimwengu wala kanuni za imani za kanisa.

95 Inanikumbusha. Siku moja wao, kwenye ki—kitalu, walisema walikuwa na bata aliyekuwa akiwafuata vifaranga wa kuku. Ndipo hu—huyo bata, mwajua, alikuwa ni jamaa wa kuchekesha kwa hao vifaranga wa kuku. Kidogo alikuwa ni mnene juu, mwajua, na domo kubwa, mwajua. Lakini hilo, akiwa ni mnene juu, a—alikuwa na hilo domo pale kwa kusudi fulani. Na hivyo ndivyo nadhani wakati mwingine Mkristo anaonekana kidogo, anakuwa na ushabiki kidogo, lakini—lakini hilo liko hapo kwa kusudi fulani. Mnaona? Kwa hiyo, yeye, kweli lilionekana ni la kuchekesha mradi tu alikuwa akikimbia huku na huku pamoja na hao vifaranga wa kuku, naye angeweza... mabata mzinga na kadhalika, wa—wa—walikuwa na midomo midogo mifupi, na wao, na wakati vitu walivyofanya, wala hawakujengwa kama huyo bata. Siku moja mama alimwongoza, pamoja na kundi la vifaranga wa kuku na yeye, huko nyuma. Sikuzote alikuwa nyuma kwa mbali, mwajua, kwa namna fulani. Hata hakuzungumza kama wao. Lugha yake ilikuwa tofauti. Wasingeweza kuelewana.

96 Hivyo ndivyo ilivyo kwa Mkristo anapozaliwa mara ya pili, mnaona. Yeye alitoka kwenye yai tofauti, hivyo tu. Mnaona? Labda ana ninii...Ninaamini kunao wengi wao huku nje kwenye makanisa haya ya kimadhehebu, ambao ni mabata halisi, bali wanaye kiongozi kuku. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kamwe hawalipati Hilo. Hilo linasikika fidhuli. Silimaanishi jinsi hiyo, bali ninajaribu kutoa hoja.

97 Siku moja akamwongoza nje kidogo mbali sana nyuma ya kitalu. Palikuwapo na maji yaliyokuwa yakitiririka nyuma ya hicho kitalu. Naam. Chemchemi ikitoka, kijito. Naye alikuwa akienda kule akishangaa kwani yote yanahusu nini, mwajua, akimfuata huyo kuku. Ndipo, mbona, hata hakupendezwa na mlo waliokuwa wakila, haukuonekana sawa kwake. Mambo haya ya kale wanayofanya, hayakuonekana sawa. Basi baada ya kitambo kidogo ilitokea alivuta pumzi. "Harufu hiyo ni nzuri. Hiyo ilitoka wapi?" Loo, maskini harufu hiyo ya Mbinguni, hummm! Pata harufu hiyo ndogo ya kitu ambacho kinaburudisha, mahubiri yanayokuvutia, yanayogonga ndani, unalihisi Neno likijitia nanga Lenyewe. Hummm, mwangaza wa jua la Mbinguni! Akawazia, "Loo, kwa njia moja ama nyingine, harufu hiyo niliyopata, inaendana na asili yangu." Akaivuta tena. "Iko mahali fulani. Sasa, huwezi kuniambia; iko mahali fulani. Ninajua kuna kitu fulani mahali fulani ambacho mimi ni wake," si wa kanuni hii ya imani. Mnaona? Mnajua ninalomaanisha? Akanusa maji, nayo asili yake ilikuwa ni bata, kwa hiyo bata na maji huenda tu pamoja. Hivyo ndivyo mwaminio na Mungu wanavyoenda pamoja. Moja kwa moja akapata mpumuo wake mwingine mkubwa, akawa

na nguvu zaidi. Baada ya kitambo kidogo upepo ukaanza kuvuma. Kama ule Upepo wa nguvu ukienda kasi, mwajua. Ukaanza kupulizia upepo mwanana moja kwa moja kutoka majini, kwake. Asingeweza kuvumilia zaidi. Huyo akatelemka kilimani, akiyumbayumba, akiyumbayumba, akiyumbayumba, akiyumbayumba, tu, mwajua, akienda, "Kok-kok, kok-kok, kok-kok." Maskini mdomo huo mdogo ukichomoza hewani, mwajua. Yeye alinusa maji!

98 Maskini yule kuku akasema, "Ewe mlokole, rudi hapa!" Halikufaa kitu; tayari alinusia maji. Alikuwa akienda zake kwenye maji!

99 "Kuna chemchemi iliyojaa Damu, iliyotolewa kwenye mishipa ya Imanueli, ambapo wenye dhambi hutumbukia chini ya hiyo gharika na kupoteza waa lao lote la hatia." Mkristo halisi hataki uhusiano wowote na ulimwengu. Hawataki kuishi mahali hapa bila mpangilio na kushangaa mahali walipo, na leo hii wao ni Methodisti na kesho ni Baptisti, na Presbiteri na Wapentekoste, na kadhalika. Ee, ndugu, hiyo ni taabu kubwa! Mkristo halisi anataka kupata usafi wa Roho, usafi wa Mungu maishani mwake, kitu kinachomfanya kiumbe kipya. Mara anapoweza kupata mlango huo, ataendesha kwenye maeneo ya theluji ama chochote kile kuipata. Huyo ataenda, kwa kuwa yeye ni bata kwa kuanzia. Naam. Si kanuni ya imani, la, la, la, la.

100 Na endapo ungali unayapenda mambo ya ulimwengu, wewe umedanganyika, dhabihu yako haijakubalika bado, asili yako haijabadilika. Sasa unajua maana ya kuzaliwa mara ya pili? Mnaona, asili yako inabadilishwa, unakuwa kiumbe kipya. Huna budi kufa kwanza, kisha uzaliwe mara ya pili. Ninajua wakati wangu wa kufunga umewadia, bali nipeni tu dakika chache, nitapitia kwenye mafungu haya upesi sana, mnaona, mnaona. Kama ungali unapenda ulimwengu, na kudai umezaliwa mara ya pili, haidhuru umefanya nini . . . Huenda ulilia, huenda upepo baridi ulipitia ndani yako. Hayo ni sawa, sina chochote dhidi ya hayo. Wakristo hulia na kuwa na upepo baridi ukipitia ndani yao. Nawe unasema, "Ndugu Branham, nilinena kwa lugha ninii tu . . . " Hilo huenda likawa ni sawa, na hilo huenda likawa ni zuri sana sikuzote.

101 Ninamwangalia maskini mwanamke mmoja sasa hivi aliyenijia sio muda mrefu uliopita pamoja na ono ama ndoto aliyokuwa nayo, nami nikapata tafsiri yake. Hata hivyo, kidogo ni vigumu kumwambia maskini mke huyo wa mhubiri wa Kipentekoste kwamba hakuwa na Roho Mtakatifu, uh-huh, bali hakuwa naye. Lakini hata hivyo akampokea, mnaona.

102 Naam, ni tofauti, mnaona. Naam, sio kunena kwa lugha, sio kucheza dansi katika Roho. Hakuna lolote la mambo hayo unayoweza kuliwekea. Ni mauti na Kuzaliwa, asili iliyobadilishwa, mwelekeo uliobadilishwa. Mambo ya kale

yamekufa, mambo mapya ni mapya; ulimwengu umekufa na Mungu ni mpya. Mungu ndiye Uzima wako, nao ulimwengu umekufa kwako. Sasa mnalipata? Vema.

103 Sasa sikilizeni. Itanibidi kukatakata kidogo hapa, mwajua, kuiondoa michongoma njiani. Wanawake na wanaume ambao hawatalifuata Neno la Mungu wala Mafundisho Yake wakiisha kudai wamezaliwa mara ya pili, kuna kasoro fulani. Nitazungumza na wanawake kwa dakika moja tu. Kama mwanamke anayejua ya kwamba Neno la Mungu linahukumu kukata nywele na kuvaa kaptura, kuvaa suruali ndefu, kuvaa kizinifu, wala hana uadilifu wa kutosha kuachilia nywele zake zikue na kuvaa nguo zinazoonekana kama Mkristo, umedanganyika. Sijali yale umepitia. Huenda umenena kwa lugha kama kumwaga njegere juu ya ngozi kavu ya ng'ombe. Huenda ulifanya, huenda ulicheza dansi katika Roho mpaka ukalitikisa jengo lote. Hilo halina uhusiano wowote nalo. Inaonyesha ya kwamba upendo wa ulimwengu ungali ndani yako. Wakati Mungu analihukumu hilo! Yeye alisema, "Sio... Mwanamke anapaswa kuwa na nywele ndefu. Nayo maumbile yenyewe yanawafundisha ya kwamba mwanamume anapaswa kuwa na nywele fupi, kwa sababu Mungu yuko juu ya mwanamume, na mwanamume juu ya mwanamke." Basi kama mwanamke akizikata nywele zake, yuaaibisha kichwa chake, ambacho ni mume wake. Kama mwanamume akiachilia nywele zake zikue, basi yuaabisha kichwa chake, ambacho ni Kristo. Mnaona? "Wanawake wenu na wajivike mavazi ya kujisetiri," safi, yanayoonekana ya mama mwenye heshima. Mnaona?

104 Halafu pasipo na uadilifu wa kawaida kufanya hivyo, sisi tunasema, "Utukufu kwa Mungu! Haleluya! Nilinena kwa lugha. Haleluya! Utukufu kwa Mungu!" Hiyo inaonyesha roho hiyo mle ndani ni mbaya. Italikubali Neno kila wakati kama ni asili ya Neno. Nalo Neno ni mwili, na Neno lilikuwa Mungu, na Neno ni Mungu; nayo Maneno yako ndani yako, yanakufanya kuwa mwana au binti wa Mungu, uzao Wake, ukiliamini Neno la Mungu.

105 "Siamini katika maskini Jina hilo la Bwana Yesu, kubatizwa katika hilo. Haleluya! Sijali unajaribu kulielezea kiasi gani, mimi ninamwamini mchungaji wangu." Endelea, huyo ndiye baba yako. Lakini iwapo Mungu ndiye Baba yako, utajilainisha na Neno la Mungu.

106 Mhubiri: "Wengi watakuja Kwangu siku hiyo, waseme, 'Bwana, mimi sikutoa pepo katika Jina Lako?' Wahubiri. 'Mimi sijafanya kazi nyingi kuu?' Wainjilisti hudumani. 'Ondokeni Kwangu, ninyi mtendao maovu,'" watoto haramu. Hiyo ni kweli.

107 Kama umezaliwa na Mungu, umeoshwa katika maji ya Neno, ukatenganishwa na mambo ya ulimwengu, na unamwamini Mungu. Wewe umekufa. Umekufa kwa fikira zako mwenyewe,

umekufa kwa mawazo yako mwenyewe, umekufa kwa kila kitu ila Neno la Mungu; na Yeye anaishi ndani yako, akitenda kazi kupitia kwako, akithibitisha kwamba ni Neno la Mungu. Unasema, "Mimi nimekufa kwa u-. . .Mimi nimekufa kwa ulimwengu, Ndugu Branham." Kisha ulikane Neno la Mungu?

108 Yesu alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Sasa tunashuka kufikia kwenye kile "kuzaliwa mara ya pili" kunachomaanisha. Mnaona?

109 Ungali una hasira, ungali ni mchoyo, mwenye kiburi. Mtu fulani akisema jambo fulani juu yako, mara moja umesimama tayari kupigana. Halafu basi, ati umezaliwa kwa Roho wa Mungu? La. Roho wa Mungu hafanyi hivyo. La. Roho wa Mungu ni mnyenyekevu, mpole, mtamu, mvumilivu. Huyo ni Mungu, mwenye upendo, ni mwema, anasamehe, huyo ndiye Roho wa Mungu. Loo, naam.

110 Bali watashikilia kwenye dhehebu hilo na kunena kwa lugha, kutabiri, kufanya kila namna ya kazi. Yesu alisema wangefanya jambo hilo. "Wenye mfano wa utauwa." Wanashikilia dhehebu kwa sababu ndilo baba yao. Walizaliwa katika baba huyo wa kimadhehebu. Bali kama umezaliwa na Mungu, *Hili* ndilo Baba yako, Yeye ni Neno, Neno. Haijalishi una mihemko mingapi, ungali ni mtoto wa Shetani mpaka utakapokuwa umeufia ulimwengu na hai katika Kristo. Sikilizeni, upesi sasa.

111 Nafsi, iwe nzuri ama mbaya, mauti hayaibadilishi. Nilikuwa na Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa kuhusu hili niliyotaka kuyafafanua, "kwamba nafsi ni nini." Nafsi ni nini? Ni wewe. Wewe ni nafsi. Ile sehemu iliyo ndani yako. Ndipo wakati utakapokufa, hali yoyote hiyo nafsi iliyomo, hivyo ndivyo inavyoenda. Inaenda kwenye kikomo chake. Usingeweza kuivuta irudi hata uifanyie nini, nafsi hiyo haina budi kubadilishwa hapa, kuzaliwa mara ya pili.

Unasema, "Vipi kuhusu Roho Mtakatifu, Ndugu Branham?"

112 Roho Mtakatifu hukubatiza katika ule Mwili, kwa ajili ya utumishi, lakini wewe unaamini hata Uzima wa Milele. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka, *yuna* Uzima wa Milele." Mnaona? Ndipo unabatizwa na Roho Mtakatifu katika ule Mwili, kwa ajili ya madhihirisho ya zile karama, na kadhalika, bali unaamini hata Uzima wa Milele. Yeye aaminiye yuna Uzima wa Milele. Na wakati unapoamini ni wakati wewe umekufa, na kuzaliwa, kufanywa upya, kiumbe kipya. Vema.

113 Nafsi, sasa kumbuka, iwe ni nzuri ama mbaya, mauti hayana uhusiano wowote nayo. Mauti huipeleka tu kwenye kikomo chake. Mnasikia hilo? Basi kama ungali una ulimwengu na kuupenda ulimwengu ndani yake, itakufa pamoja nawe, maana ulimwengu hauna budi kufa. Mungu ameuhukumu ulimwengu,

huo ni utaratibu wa ulimwengu. Mungu ameuhukumu nao hauna budi kufa. Basi kama ulimwengu huo uko ndani yako, wewe utakufa pamoja na huo ulimwengu. Jamani, sioni jinsi lingekuwa dhahiri zaidi. Mnaona? Na kama ni nzuri, iliyozaliwa na Mungu, haina budi kwenda kwa Mungu. Iwapo ni ya ulimwengu, itabaki ipate kuangamia pamoja na ulimwengu. Kama ni ya Mungu, itaishi pamoja na Mungu, iwe na elimu ama isiwe na elimu. Iwe na elimu ama isiwe na elimu, endapo ulimwengu ungali pale, haina budi kufa. Na kama ulimwengu uko ndani ya nafsi yako, nayo shauku yako ni ya mambo ya ulimwengu huu, wewe utaangamia pamoja na ulimwengu. Hiyo ni dhahiri, sivyo? Inapaswa kuwa. Wewe ni sehemu ya ulimwengu uliokufa. Basi kwa kuwa ulimwengu umekufa, wewe umekufa pamoja na ulimwengu.

114 Lakini kama umezaliwa mara ya pili, wewe u hai pamoja na Kristo, nao upendo wako uko kwenye mambo yaliyo juu wala si kwenye mambo ya ulimwengu. Lakini kama umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, unakuwa sehemu ya Mungu nawe ni wa Milele pamoja na Yeye. Ndipo, mauti hayawezi kukugusa wakati umezaliwa mara ya pili. Wewe ni wa Milele. Umebadilika kutoka kwenye kiumbe cha wakati ukawa kiumbe cha Milele. Umebadilika kutoka mautini ukaingia Uzimani. Ninazungumza kuhusu "Milele." Kutoka kwenye mauti ya Milele hadi kwenye Uzima wa Milele. Endapo wewe ni wa ulimwengu, unakufa hapa pamoja nao. Ukipenda . . . Biblia ilisema, katika Yohana, "Ukiipenda dunia au mambo ya dunia, ni kwa sababu kumpenda Mungu hata hakumo ndani yako." Huwezi kuipenda dunia. Naye Yesu alisema, "Huwezi kumpenda Mungu pamoja na mali." *Mali* ni "ulimwengu." Huwezi kuipenda dunia na Mungu wakati uo huo. "Naye asemaye kwamba ananipenda Mimi, wala hayatii maneno Yangu," hiyo ni kusema, Biblia, "yeye ni mwongo, na Kweli hata haimo ndani yake." Haya basi.

115 Loo, Maskani ya Branham, nanyi nyote watu wazuri, hebu tufanye hesabu! Huu ni Mwaka Mpya. Hebu tuanze, hebu tufanye jambo fulani, tuyaondoe mambo ya ulimwengu kutoka kwetu. Kama yangali mle ndani, hebu tuyaondolee mbali. Naam, bwana. Vema, watu wa siku hizi . . . Sina budi kuharakisha.

116 Watu wa siku hizi huchukua kila namna ya roho. Wanaenda na kuchukua roho ya kanisa, hata wanachukua roho zinazojiita "roho za Mungu, ati wamezaliwa mara ya pili," na kulikana Neno la Mungu kuwa ni kweli. Ungeweza kuwazia Roho wa Mungu akilikana Neno Lake Mwenyewe? Kwenu ninyi Wakatoliki, Wakatoliki wa Kirumi, ninamaanisha, kweli mngeweza kusema kwamba mmezaliwa kwa Roho wa Mungu, na kuyachukua mafundisho hayo ya sharti ambayo ni kinyume na Biblia, na kulikana Neno la Mungu, na kusema ya kwamba ninyi ni . . . Roho wa Mungu yuko ndani yenu? Ati Roho aliyeiandika Biblia hii angeikana? Hiyo ingekuwa ni mimi nikisema jambo

fulani kisha nisimame na kudanganya dhidi yake. Ati Mungu aseme jambo fulani, kisha ageuke na kulidanganyia? Wakati Biblia ilisema, "Haiwezekani Mungu kusema uongo, maana Yeye ndiye Chemchemi hasa ya Kweli yote."

117 Ninyi Methodisti, Baptisti, mliobatizwa katika vyeo vya "Baba, Mwana, Roho Mtakatifu," nanyi mnajua tofauti sasa? Mnayo Biblia yenu. Ninyi ambao mnachukua tu kujiunga na Kanisa, kwa kupeana mkono? Wewe unayepeleka barua yako kutoka moja hadi lingine, na kudai kwamba umezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu? Unawezaje kufanya hivyo, kisha uangalie usoni pa Neno la Mungu na kujiita Mkristo aliyezaliwa mara ya pili? Wakati unapolifia kanisa, umekufa kwa kanuni za imani, umekufa kwa ulimwengu, umekufa kwa kila kitu kingine ila Mungu, naye Mungu ni Neno! Haya basi. Hebu tuone. Wao wanachukua kila namna ya roho. Loo, wana roho za kanisa, wana kila namna ya roho. Sasa sikilizeni kwa makini.

118 Manabii! Neno la Mungu humjia nabii. Biblia ilisema hivyo. Sasa, katika kufunga, ninayo matamshi mengine machache tu hapa, ama hivyo, ninayotaka kuwapa, na kisha nitakata. Neno la Mungu liliwajia manabii. Ni kitu gani kilichowajia manabii? Neno la kanisa liliwajia manabii? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Neno la kanuni ya imani lilimjia nabii? ["La."] Neno la Bwana! Ilikuwa ni kitu gani? Nabii alilifunua Neno la Mungu. Mnaona? Hao ni manabii, manabii halisi. Sasa, tunao manabii wa uongo, tunawaendea kwa dakika moja tu. Bali nabii wa kweli, Neno la kweli lilimjia nabii wa kweli. Lisingeweza kuwa kitu kingine chochote. Sasa, kanuni ya imani haikumjia nabii, dhehebu halikumjia nabii. La. Lakini Neno la Bwana lilimjia nabii, naye akalifunulia watu. Nabii wa kweli alikuwa na Neno la kweli.

119 Unamjaribuje nabii wa kweli? Wakati akiwa na Neno la kweli. Ndipo kama si Neno la kweli, halina budi kuwa ni la uongo. Kama likisema jambo fulani tofauti na Neno hili, nalo Neno hili ni Neno la Mungu, neno la kila nabii na liwe uongo nalo Neno la Mungu liwe ni kweli. Na kama Neno hilo linatoka kwa nabii, ni Neno la Mungu, basi yeye ni nabii wa kweli, kwa sababu Neno huja kwa manabii, manabii wa kweli. Daima tumekuwa na wa uongo. Manabii wa kweli, Neno la kweli. Manabii wa uongo, neno la uongo, "kanuni zetu za imani, madhehebu yetu, jiunge na *hili*, sema *hili,* amini *hili,* fanya *hili*."

120 Lakini Neno la kweli humjia nabii wa kweli, naye anakwambia Neno la kweli. Wewe lifuate Neno hilo la kweli, na unapata ujuzi wa kweli wa Neno kwa sababu Neno limefanyika mwili ndani yako, nawe unakuwa mwana wa Mungu, nalo Neno la Mungu linazunguka moja kwa moja kutoka kwa Mungu linaingia ndani yako, kwa sababu wewe ni Asili Yake, Roho Wake yumo ndani yako nawe utazifanya kazi za Mungu. Haleluya! Biblia ilisema hivyo. Loo, jamani!

121 Manabii wa uongo huleta maneno ya uongo. Wanafanya nini? Wana mihemko ya uongo. Manabii wa uongo hushika Neno la kweli la kutosha wapate kuwa wa uongo. Hawakuwa wakifanya hivyo, bali Biblia ilisema . . . Mkitaka kuyaandika Maandiko juu ya hilo, Timotheo wa Pili 3, mnaona. Manabii wa uongo wana Neno la kweli la kutosha kulifanya la uongo, kwa sababu Biblia ilisema kwamba wangekuwa na "mfano wa utauwa." Kusudi wawe na mfano wa utauwa, hawana budi kuwa na baadhi yake kama Kweli. "Mfano wa utauwa, bali wakikana nguvu zake." Nguvu za nini? Kukufanya unyoke, uwe tofauti, ukamtumikie Mungu, sio kwenda kwenye madansi na mambo ya ulimwengu, Biblia inahukumu, usizikate nywele zako. Kama vile, manabii wa uongo wanasema kwamba, "Haileti tofauti yoyote."

122 Mtu fulani alisema sio muda mrefu uliopita (Ninaamini nililinukuu hilo hapa hapo awali, sijui) kasema, "Kwa nini kamwe usiachane na hao wanawake na wanaume," kaniambia. Kasema, "Mbona, hapo, watu wanakuamini wewe kuwa ni nabii."

Nikasema, "Mimi siye."

123 "Lakini watu wanakuamini kuwa ndivyo ulivyo. Kwa nini usiwafundishe jinsi ya kupokea maono, jinsi ya kufanya kazi za Mungu namna hiyo?"

124 Nikasema, "Ninawezaje kuwafundisha aljebra wakati hawajui ABC zao?" Mnaona? Mnaona? Unawezaje kumtoa mtoto kwenye shule ya chekechea na kumpa elimu ya chuoni leo hii, ati umfundishe kipimo cha kipeo cha pili? Unawezaje kufanya hivyo wakati hajui maana ya *ABC*? Mnajua *ABC* zinamaanisha nini? "Daima Mwamini Kristo." [Kiingereza: Always Believe Christ—Mf.] Hiyo ni kweli. Usiliamini kanisa, usiamini kanuni ya imani, usiyaamini mafundisho yao. Mwamini Kristo! Kwa nini? "Kumjua Yeye, kumjua Yeye ni Uzima." Hiyo ni kweli? Sio kujua kanuni Yake ya imani, sio . . . Yeye hana kanuni zozote. Sio hata kulijua Neno Lake. Sio kulijua Neno Lake; inakupasa kumjua Yeye, kumjua Yeye kama Mwokozi wako katika kuzaliwa upya. Kama Yesu alivyomwambia Nikodemo, "Kama huwezi kuamini mambo ya duniani ninayokuambia, ungewezaje kuamini mambo ya Mbinguni?" Mtaaminije mambo ya kiroho yanayoingia Rohoni, na kujua na kuona maono na mambo kama hayo, kuiweka shule katika utaratibu jinsi hiyo, wakati hata hawaamini mambo ya duniani? Hata hawawezi kuamini kuvaa nguo vizuri. Hata hawawezi kuamini kuacha kuvuta kwao sigara na kuacha kusema kwao uongo, kuweka hamaki yao kando, na mambo hayo yote, kufanya mambo haya yote, ama kuacha kushikwa na tamaa. Unawezaje kuwafundisha watu kuingia katika Roho wakati wana mambo haya yote yakining'inia juu yao? Naam. Loo, jamani.

125 Manabii wa uongo wana maneno ya uongo, kanuni za imani,

madhehebu, mihemko. “Loo, Mungu abarikiwe, jambo pekee likupasalo kufanya. Unataka kuvaa vazi la Eliya? Utukufu kwa Mungu! Jambo pekee likupasalo kufanya ni kujifanya tupu niani mwako, usiwazie jambo lolote, na kusema, ‘Loo, nijaze, nijaze, nijaze.’” Ibilisi hakika atakujaza. Halafu unategemea hilo? “Loooo, ilipitia kote juu yangu, Ndugu Branham. Niliihisi. Loooo, utukufu kwa Mungu. Haleluya!” Ukiruka juu chini namna *hiyo*. “Loo, ninaye.” Kisha uishi jinsi unavyoishi?

126 “Kwa matunda yao mtawatambua.” Mnaona? Mnaona, sio mhemko.

127 “Loo, ndugu, ukitaka kumpokea Roho Mtakatifu, shuka tu uende madhabahuni na kusema, ‘Utukufu, utukufu, utukufu, utukufu, utukufu, utukufu, utukufu, mpaka unene kwa lugha.’” Uh-huh, unarudi na kuishi namna yoyote ya maisha, unadanganya, unaiba? Wanapokwambia kuhusu kubatizwa katika Jina la Yesu Kristo, “Huo ni ulokole, kanisa langu hufundisha vinginevyo!” Na kusema ati umezaliwa mara ya pili, ukaoshwa kwa maji ya Neno? Kasoro fulani mahali fulani. Mnaona?

128 Utaamini kila Neno jinsi tu lilivyoandikwa hapa. Hatuhitaji. . .wala hatuninii. . .Nayo Bi—Biblia ilisema, “Si ya kufasiriwa apendavyo mtu binafsi.” Mungu aliifasiri, na hivi ndivyo ilivyo. Yeye. . .Neno, Neno Lake hapa. Hivi Biblia haisemi katika nanii wa Pili. . .ninaamini Petro wa Pili hapo, “Biblia si ya kufasiriwa apendavyo mtu binafsi.” Hakika. La, hakuna fasiri ya kibinafsi. Imeandikwa jinsi tu inavyolimaanisha Hilo, moja kwa moja namna hiyo. Iamini tu jinsi tu ilivyoandikwa hapa, italeta matokeo yale yale.

129 Sasa, walimu wa uongo wataleta kuzaliwa kwa uongo. Manabii wa kweli watalileta Neno, kuzaliwa kwa Neno, Kristo. Manabii wa uongo wataleta kuzaliwa kwa uongo, kuzaliwa kwa makanisa, kuzaliwa kwa kanuni za imani, kuzaliwa kwa madhehebu. Nawe huyu hapa, ndugu wa Kipentekoste, ninii ya uongo. . .ama mihemko, na kumwambia mtu anaye Roho Mtakatifu maana hunena kwa lugha. Nimewaona ibilisi wakinena kwa lugha; penseli zikiwekwa chini na kuandika katika lugha zisizojulikana. Hilo halimaanishi kitu. Mnaona, inapaswa kuwa ni maisha, kwa matunda yao mtawatambua. “Ndugu Branham, unaamini katika kunena kwa lugha?” Naam, bwana. “Unaamini katika kupaza sauti?” Naam, bwana. Kusudi niwe Mkristo, ninaamini hilo. Ninaliamini Neno la Mungu. Bali kama maisha hayako kuliunga mkono!

130 Unatoka huko nje umejaa kiburi, “Utukufu kwa Mungu. Haleluya!” Na halafu uniambie ya kwamba huyo ni Kristo? Kristo alikuwa asiyetaka makuu, mnyenyekevu na mpole. Unaingia mjini na, jamani, huna budi kupigwa brashi mabegani, mwajua, na kila kitu hakina budi kuwa sawa kabisa, hakuna kunyanzi kwenye suti yako, na inakubidi kuwa na mazuri kuliko

yote la sivyo kamwe hutakuja, usipohakikishiwa kiasi fulani cha pesa; huwezi kufanya mkutano. Loo, loo, loo, loo, loo, jamani! Madhehebu yote, hayana budi kukupapasa mgongoni. Hapakuwapo na moja la hayo lililompapasa Yeye mgongoni, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Neno. Hiyo ni kweli.

131 Wa uongo huweka kweli ya kutosha kufanya mfano wa utauwa. Basi sikilizeni, sasa ninasema jambo fulani hapa, ninawatakeni msikilize. Namna hizo za dhana za uongo, mnajua dhana ya uongo ni nini, huwaongoza mamilioni ya watu kwenye kuzaliwa kwa uongo. Walimu wa uongo huwaongoza watu kuamini katika mhemko, "Maana ulitetemeka kila mahali, unaye. Loo, kwa sababu ulipata hisia za ajabu sana zilizopita mwilini mwako mwote, u—uliona nuru mbele zako, kisha ukawa kipofu na ukapepesuka, hilo ni koti la Eliya ulilovalishwa. Hiyo ni kweli, umempata. Loo, unajua wewe ni nini? Wewe ni mwana wa Mungu aliyedhihirishwa." Unajikuta wapi? Umeshindwa. Hiyo ni kweli. "Utukufu kwa Mungu, nilienda usiku mmoja na nikaota ndoto!" Loo, naam, uh-huh. Mnaona? "Loo, niliona *hili, lile*." Naam, uh-huh. "Wewe, kwani huamini katika ndoto?" Naam, bwana, bila shaka ninaamini. Lakini kama ndoto hiyo hailiungi mkono Neno la Mungu, basi ni ya uongo. Hii ndiyo Kweli hapa, dumu kwenye *Hili*. Naam, bwana. Kuwaongoza mamilioni kwenye kuzaliwa kwa uongo, wazia tu!

132 Nina kipande cha karatasi nilichotaka kukileta, ambapo baba wa ekumenia wa Othodoksi yote ya Kiyunani na makanisa ya Kiothodoksi yamezungumza na Papa Yohana wa 22, naye akasema, "Huenda tusilione katika kizazi chetu, bali ule udugu mkuu katika muungano wa Protestanti na Katoliki unaungana pamoja."

133 Nikawazia, "Mungu asifiwe!" Mtu fulani alikikata kwenye gazeti, akaniandikia namna hiyo. Ninaamini ilikuwa ni Ndugu Norman ama mtu fulani, aliyesema, "Ndugu Branham, imechelewa kuliko tunavyodhania." Angalieni siku hizi, waziri wa vita na, loo, ofisi nyingi sana mbalimbali pamoja na Rais, nalo taifa hili lote linatawaliwa na Katoliki. Sikilizeni!

134 Mnasema, "Vema, hao ni Wakristo." Kuwa Mkristo ni kuwa kama Kristo, kuwa na Roho Wake. Hiyo ni kweli? Hili hapa fidhuli, jambo fidhuli, bali ninataka kulisema. Kama ungalimwita nguruwe kondoo hiyo ingemfanya kondoo? Mbona, kama ulisema, "Nguruwe, nimechoshwa kabisa na wewe kuwa nguruwe. Ninataka mwana-kondoo, kwa hiyo nitakupeleka hapa nje nami nitakusugua kabisa, nami nitayaosha meno yako, kisha nitazichana nywele zako kabisa, na mimi—mimi nitakufanya mwana-kondoo mdogo. Nitakufungia riboni ndogo ya zambarau shingoni mwako nawe utakuwa maskini mwana-kondoo badala ya nguruwe." Ukija huku na kusema, "Mwana-kondoo, mwana-kondoo, mwana-kondoo," angali ataenda, "Oink, oink." Ukimwachilia kwenye kizimba cha nguruwe,

atakula uchafu wote awezao kupata. Kweli! Sio kumnyunyizia, sio kumweka majini; ni mauti na kuzaliwa! Naam, bwana. Useme, "Sitakulisha chochote ila alfalfa, nitakulisha chakula cha kondoo." Hata umlishe alfalfa, yeye angali ni nguruwe. Hivyo tu. Hiyo ni kweli? Bila shaka ni kweli. Mbona, hakika, yeye ni nguruwe kwa sababu asili yake ni nguruwe.

135 Na kama ukiupenda ulimwengu ama mambo ya ulimwengu, wewe ungali ni nguruwe. Hiyo ni kweli. Inahitaji nguvu za Mungu kuibadilisha hiyo nafsi. Kufa nguruwe, weka tabia zako za nguruwe kwenye madhabahu, jilaze mwenyewe mle, na uache dhabihu ya Mungu iwe. . . ama moto wa hukumu ushuke chini na kukumeza, kama nguruwe, na kukuzaa tena kama mwana-kondoo. Ndipo hutakula takataka yoyote, usingeweza, ulaji wako hautaimeng'enya. Huko sawa. Haitaninii, bila shaka haitamfanya ngu—nguruwe kusema. . . ama kumfanya mwana-kondoo kusema yeye ni mwana-kondoo.

136 Vivyo hivyo mtu anayeitwa Mkristo, kwa kanuni fulani za imani ama mhemko fulani! Unasema, "Utukufu kwa Mungu, Ndugu Branham, nilicheza katika Roho usiku kucha usiku huo. Nilinena kwa lugha, loo, jamani, Ndugu Branham!" Ninazungumza na Wapentekoste sasa. "Ni—ni—nilicheza katika Roho. Loo, nilikuwa na mihemko, kila kitu namna hiyo. Lakini nakwambia sasa hivi, usiendelee kunizungumzia juu ya upuuzi huo hapo wa Jina la Yesu." Endelea, nguruwe. Ungali nguruwe, hivyo tu.

137 "Kondoo Wangu hulisikia Neno Langu!" Ninasema, "Lakini, ndugu, angalia, nitafutie mahali pamoja ambapo walipata kubatizwa 'katika jina la Baba, Mwana, Roho Mtakatifu,' katika Biblia."

138 "Sijali yale hilo lifanyayo, haleluya, sitaki yoyote ya maskini upuuzi huo wa Yesu Pekee." Ni nani aliyesema lolote kuhusu upuuzi wa Yesu Pekee? Ninazungumza kuhusu Biblia. Yesu Pekee ni lundo la kanuni za imani na kundi la madhehebu. Mmoja hawezi kumwita huyo mwingine kitu kingine, maana wote wako ndani yake.

139 Lakini ninazungumza kuhusu Wakristo kwelikweli, halisi, asilimia mia moja, waliozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, na matone ya umande wa Mbinguni maishani mwao. Hilo ndilo ninalozungumza habari zake. Kama wewe ni Mmethodisti na una hilo, amina! Jambo pekee linalokupasa kufanya ni kuelekezwa kwenye Neno, utalifuatilia kama bata akienda kwenye maji. Mnaona? Kweli kabisa. Hiyo ni kweli.

140 Watu siku hizi wanataka njia za mkato. Hawataki. . . wao—wao wanafikiri unampata katika dakika moja tu, "Utukufu kwa Mungu!" Ni kitu gani? Ni kitu gani wanachofanya? Usiku wa leo wako katika—wako huko nje katika. . . Kama baadhi ya hawa jamaa walio nao kama watu fulani ambao ningeweza

kuyataja majina yao, bali sitaki kufanya hivyo kwa sababu huu uko kwenye kanda, bali wako kwenye kilabu ya usiku usiku wa leo wakiwa na gita, wakiicheza, na kesho asubuhi wamesimama kanisani mahali fulani, wakiicheza gita iyo hiyo. Uchafu! Biblia ilisema katika Isaya, mlango wa 28, "Meza zote zimejaa matapiko. Kama vile mbwa aendavyo kwenye matapiko yake na nguruwe kwenye kugaagaa kwake, vivyo hivyo na wao." Kwa nini? Wangali ni mbwa na nguruwe! Hilo ndilo linalowafanya warudi kwenye kugaagaa na kwenye matapiko. Ungali ni. . .Hawajazaliwa mara ya pili. Kama wamezaliwa mara ya pili, wao ni viumbe vipya.

141 Unajua nini? Una maskini kunguru wa kale, yeye—yeye. . . haijalishi ni kiasi gani unajaribu kuninii. . .ungeweza kumpaka rangi ya—ya kizeituni tu kama hua, ya kijivu tu kama hua, nyeupe, umpake rangi kila mahali, yeye angali ni kunguru ndani. Mnaona? Angali ananuka, koho wa kale vivyo hivyo, mla mizoga, anakula vitu vilivyokufa vya duniani. Hiyo ni kweli. Bali unajua nini? Hua hata haimbidi kuoga. Loo, haleluya! Mwili wa hua, kwa sababu yeye ni hua, yeye anayo mafuta ambayo huja kupitia kwenye manyoya yake, yanayomweka safi wakati wote, kwa sababu yanatoka ndani yakienda nje. Loo! Kwa nini? Koho asema, "Yangu, pia! Niliweka maji matakatifu kidogo, ndugu, yalilitengeneza." La, hayakulitengeneza. Kwa kuwa, yanatoka ndani kuja nje, sio kutoka nje kwenda ndani. Ni kuzaliwa. "Mungu abarikiwe, mimi huenda kanisani kama wewe uendavyo. Haleluya, kanisa langu ni zuri tu kama lako lilivyo. Haleluya, tunaninii tu. . ." Vema, ewe koho. Mnaona, hiyo ni kweli. Mnaona? Lakini hua anatiwa mafuta kutoka ndani. Kuna te—tezi fulani katika hua ambayo haiko katika ndege mwingine namna hiyo, hua ama njiwa. Naye hujipaka mafuta kutoka. . . Nje, yeye hujiweka safi wakati wote. Haimbidi kujiweka safi, kuna kitu ndani yake kinachomweka safi. Loo, Dada Way. Haleluya! Kitu fulani ndani yake humweka safi.

142 Unasema, "Ninajua, nilijiunga na kanisa wiki jana. Ha—ha—hakika ningependa kunywa hicho kinywaji pamoja nawe, lakini, huh! Umm, hiyo sigara inanukia vizuri sana! Loo, dada, najua mimi ni wa mtindo wa kale, sina budi kuziacha nywele zangu zikue sasa. Si ni vibaya sana? Mnajua hizo nguo nzuri fupi nilizokuwa nikivaa, na kila mtu akasema, 'Whiu-whiu,' Inanibidi kuzitoa sasa. Mwajua, nilijiunga na kanisa juma lililopita." Maskini mnyonge wee! Maji yote matakatifu ulimwenguni yasingaliweza kukusafisha.

143 Lakini, ndugu, unapopata kitu Fulani ndani yako, Huisafisha kabisa wakati wote. Unasimama tu kimya na Hiyo inaosha.

144 Haikubidi kumwambia kondoo, "Huna budi kutengeneza." Hiyo ndiyo shida ya Wapentekoste leo hii. Hiyo ndiyo shida ya Ukristo wote, ni kujaribu kujitengenezea kitu fulani. Kondoo

haombwi kujitengenezea sufu; yeye huzaa sufu. Wewe unazaa matunda ya Roho. Husemi, "Utukufu kwa Mungu, sina budi kuwa mweusi usoni, sina budi kufanya *hivi,* na sina budi kupata mhemko, Sina budi kucheza katika Roho, nami nimempata." La, la, uh-huh. Zaliwa tu mara ya pili na kwa kweli litatukia lenyewe. Haikubidi kusema, "Nisome usiku kucha, nifanye *hivi,* nifanye *vile,* nijiunge na *hili,* na nifanye kanuni hii ya imani, nifanye vitubio hivi?" La, la. Kufa tu, hivyo tu. Unaona? Zaliwa mara ya pili, nayo inakuja kutoka ndani, inashughulikia yaliyo nje. Mnaona? Kuwanyunyizia maji kidogo, na kuwaosha, kama tu kumbadilisha nguruwe kuwa mwana-kondoo, huwezi kumbadilisha. Lakini kama mle ndani yeye ni mwana-kondoo, basi hatakuwa nguruwe tena. Mnaona? Hayo ni matamshi fidhuli; bali mimi sina elimu, inanibidi tu kuyatoa.

145 Mwajua, ni, nilikuwa nikiwazia, nilisoma katika maisha ya Yohana Mbatizaji hivi majuzi, yale aliyosema, yale aliyowaita, "Enyi kizazi cha majoka!" Kwa nini? Alikuzwa nyikani. Mnaona, yeye alijua kile walichokuwa. Kanyaga kwa kishindo nao watatoroka wajifiche. "Enyi kizazi cha majoka." Pia, "Shoka limewekwa penye shina la mti." Mti, majoka, mashoka, yeye alizungumza juu ya yale aliyojua. Hivyo ndivyo unavyomjua Mungu, kwa yale unayojua. Unaona nguruwe na mwana-kondoo, hakuna kitu hata kidogo. Huwezi kufanya . . . Huenda ukamwosha maskini nguruwe huyo na kufanya chochote utakacho, yeye angali ni nguruwe. Hana budi kuzaliwa tena kabla hajaweza kuwa mwana-kondoo.

146 Njia za mkato! Usiku wa leo, wako hapa nje leo hii, wanaendelea, loo, jamani, na kesho wanataka kuhubiri. Wapentekoste wakiwaachilia wafanye hivyo, pia. Naam. Wanataka njia ya mkato ya kwenda Mbinguni, "Haleluya, yote yanipasayo kufanya ni kushuka hapa wala nisiwazie kufanya lolote hata kidogo, na kusema, 'Haleluya, haleluya, nimevalia vazi la Eliya. Ninatoka nje kesho kuwatoa pepo. Haleluya, haleluya, nimelipata!' Mungu asifiwe, mimi huyu hapa ninaenda!" Wanataka njia ya mkato ya kwenda Mbinguni, wakichukua mengi ya ulimwengu kadiri wawezavyo. Huwezi kuchukua yoyote yake. Hakuna njia za mkato. Unakuja kwa njia ya Kalvari. Unakuja kwa njia ya madhabahu ya shaba. Unakuja kwa njia ya nyoka wa shaba. Unakufa! Kweli unakufa. Ee Mungu, kwa nini siwezi kulisema vizuri? Unakufa! Kikweli unajifia mwenyewe. Unakufa kwa mambo ya ulimwengu, na unazaliwa upya. Amina. Hakuna ulimwengu, mambo ya ulimwengu yamekufa. Hakuna njia za mkato. Mnaona? Wanataka kuja upesi sana, hawataki kukua. Tunakua katika Bwana. Inahitaji kukua na ujuzi.

147 Watu wanaambiwa kwenye Pwani ya Magharibi sasa, "Loo, tunao ubatizo usiopatikana na mauti. Tunakubatiza katika maji, unageuka moja kwa moja ukawa kijana

mwanamume papo hapo, msichana. Naam, bwana. Unaendelea kuwa. . . ” Wanayo mavazi ya Eliya, wanao wana wa Mungu waliodhihirishwa. “Naam, bwana, ndugu, Mungu anawapata wana waliodhihirishwa sasa hivi. Kudhihirishwa, kuwaambia yote kuhusu *hili*. Usiku wa leo wewe ni mwenye dhambi, kesho nyinyi ni wana wa Mungu waliodhihirishwa.” Upuuzi! Unapata hayo wapi kwenye Neno? Watoto wachanga hawazaliwi wakiwa watu wazima, wanazaliwa watoto wachanga kisha wanakua wakawa watu wazima.

148 Sikilizeni hapa, hebu ninukuu tu kwa dakika moja na kuwasomea kitu fulani katika Waefeso, kifungu cha 11, cha 12, yapata cha 15, ninaamini ndivyo, mahali fulani hapa ndani. Hebu tuanzie kwenye kifungu cha 12:

> *Kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu,* kazi *ya huduma itendeke,. . .mwili wa Kristo ujengwe:*
>
> *Hata na sisi sote tutakapoufikia umoja wa imani na. . .kumfahamu sana Mwana wa Mungu,* hata. . .*mtu* mkamilifu, na *hata kufika kwenye cheo cha kimo* Chake na *utimilifu wa Kristo:*
>
> *Ili tusiwe* tena *watoto wachanga, tukitupwa huku na huku, na kuchukuliwa na kila upepo wa mafundisho,* (sikilizeni, na ni mafundisho gani?) *kwa hi—hila ya watu, na kwa ujanja, ambapo* wanangojea *kukudanganya* wewe;
>
> *Lakini tukiambiana kweli kwa upendo,*. . .(na, ngojeni, nini?). . .tukiambiana *kweli* (Yeye ndiye Kweli) *kwa upendo,*. . .

Sikilizeni! Mnasikiliza? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

> (Kitu gani?). . .*kukua hata tumfikie yeye*. . .

Ati nini? Kesho? La. “Tukue hata tumfikie Yeye.”

> . . .*kukua—kukua* hata *tumfikie yeye*. . .*aliye kichwa, yaani Kristo:*

Kukua katika Yeye! Loo, kuna ninii. . .

149 Ninakumbuka mahubiri ya kwanza niliyohubiri. Nilipanda kule na ni—nikawazia nilifanya vizuri kweli, nao mama wazee wote waliketi karibu nao wakalia kidogo, mwajua, na kusema, “Loo, ni mvulana mzuri jinsi gani.”

150 Yule mchungaji mzee, Daktari Davis, alikuwa mwanasheria mzee. Nikashuka kule, naye akasema, “Nataka kukuona kule chini nyumbani.”

151 Nikasema, “Sawa.” Nikaingia, kesho yake, mwajua, huku najigamba. Nikasema, “Nilifanyaje, Daktari Davis?”

Kasema, “Ndiyo mabaya kuliko yote niliyowahi kusikia!”

Nikasema, “Ati nini?”

Akasema, "Ndiyo mabaya kuliko yote niliyowahi kusikia."

"Loo," nikasema, "Ndugu Davis, kila mtu alikuwa akilia."

152 Akasema, "Naam, wanalia kwenye mazishi, wanalia wakati wa kujifungua, mengine yote." Akasema, "Jambo ni kwamba, Billy, wewe kamwe hukunukuu hata kipande kimoja cha Neno la Mungu. Ulizungumza juu ya mama fulani aliyekuwa tayari ameaga dunia, ama kitu kama hiki, na kumfanya kila mtu kulia." Kasema, "Huzaliwi mara ya pili juu ya mambo na mihemko ya dunia hii, unazaliwa kwa Neno!" Kasema, "Billy!"

153 Loo, alinikatisha pumzi kabisa. Nina furaha kwamba alifanya hivyo. Mnaona? Mnaona? Sio kurukaruka juu chini, ukipiga makelele, hilo silo. Neno ndilo linalofanya hai. Neno limehuishwa. Sio ujuzi; Neno!

154 Akasema, "Ninakumbuka kesi ya kwanza niliyotetea, Billy." Akasema, "Nilipigapiga kwenye ubao," naye akasema, "Nikasema, 'Mtazame maskini mwanamke huyu.'" Loo, yeye akasema, "'Tazama jinsi anavyoonekana, na mumewe amemtesa.'" Kisha kasema, "Nililia kidogo kisha nikaichukua leso yangu, nami nikatenda kama hao wanasheria wengine." Kasema, "Nilifikiri ningepitia kwenye mhemko ule ule." Kasema, "Hakimu, Mheshimiwa, mbona usimpe talaka? Angalia pale! Anasema ya kwamba mumewe alimpiga mgongoni." Hata asingeweza kuliona, chini ya nguo zake za ndani. "Walimpiga mgongoni." Nami nikasema, "Kwa nini usimpe..." Maskini hakimu aliketi tu pale, akatazama.

155 Moja kwa moja mwanasheria mzee aliyeketi upande wa pili, alikuwa amekomaa, akasema, "Hakimu, Mheshimiwa, ni kiasi gani zaidi tutaninii...wa upuuzi huu mahakama yako itavumilia?" Makelele matupu tu.

156 Hivyo ndivyo watu wengi kupita kiasi wanavyofanya. Makelele mengi kupita kiasi pasipo na Neno la kutosha nyuma yake la kuyaunga mkono. Kueni! "Loo, yeye alicheza katika Roho jana usiku, Ndugu Branham, yeye yuko sawa." Hasha, hilo halimfanyi sawa kwangu mimi. La, bwana. Hana budi kukua, kuthibitishwa, kujaribiwa, kukua kumfikia Yeye, kukomaa.

157 Nilikuwa nikisoma katika historia si muda mrefu uliopita. Ninachukua muda mwingi kupita kiasi? Nilikuwa nikisoma katika historia ya kanisa. Nafikiri Dada Arnold pale nyuma aliniitikia "amina" hivi majuzi usiku juu ya jambo fulani kuhusu historia ya kanisa, ambayo alikuwa akiisoma. Niliona ambapo usiku mmoja kulikuwako na mvulana katika nyumba ya watawa, katika siku za Mtakatifu Martin, ambaye alisema, "Bwana alinifanya mimi nabii wa kale kutoka kwenye Agano la Kale. Mnaona? Mimi ni mmoja wa manabii wa kale." Vema, siwezi kulikumbuka jina la huyo askofu kule, wa shule hii, kundi dogo tu kama hili. Siwezi kulikumbuka jina lake wakati huu, lakini yeye alifunzwa chini ya Martin. Halikusikika sawa

kabisa, kwa hiyo hao ndugu wengine waliachana tu naye. Moja kwa moja akatabiri, akasema, "Usiku wa leo Mungu anashuka na atanipa mimi joho jeupe, nipate kuketi miongoni mwenu, nanyi mtajua ya kwamba mimi ni mmoja wa manabii wa Agano la Kale." Kwa hiyo usiku huo, saa sita, kweli lilitukia. Sauti zilisikika, watu wakitembea huko, naye mvulana huyo akapata joho, walisema jeupe tu lilivyoweza kuwa. Akatoka nje, kasema, "Hivi sikuwaambia?" Kasema, "Sasa ninyi nyote mtashika amri yangu. Mimi ni nabii wa Agano la Kale."

158 Lakini maskini yule askofu hakushawishika vema. Halikuwa Neno. Manabii hawafanywi, wanakusudiwa tangu zamani. Wala nabii asingefanya namna hiyo, kwanza. Tunda lake lilithibitisha ya kwamba haikuwa ni kweli. Mnaona? Hayo matunda yalithibitisha kwamba hakuwa nabii, mnaona. Kwa hiyo yeye alisema, "Tutatumia usiku uliosalia katika kufunga na kuomba, na kuimba nyimbo." Siku moja hivi ilipita. Baada ya kitambo kidogo yule askofu mzee, akiomba, alisema, "Bwana, mvulana huyo!" Vazi hilo, waliliangalia, se-. . .kamwe hawakupata kujua chochote, kuona chochote kama hilo. Waandishi wakaja wakaliangalia, wala kamwe hawakuwa wameona chochote kama hilo. Hilo hapo. Hatimaye, walimjua mtu mmoja aliyekuwa ni nabii, huyo alikuwa ni Martin. Wakasema, "Vema, jambo moja sasa utakalofanya kututhibitishia. Kimaandiko wewe umekosea. Vipi kuhusu kwenda kwa Martin na kusimama mbele yake na kumwambia hilo?" Mnaona?

Akasema, "Loo, nimekatazwa kusimama mbele ya Martin."

159 Aliye na dhahabu nzuri haogopi kwenda kwenye mtambo ya kupimia; um-hu, hiyo ni kweli, yeye aliye na Ukweli. Hiyo ndiyo sababu ninatoa changamoto: Mtu yeyote aje anionyeshe ambapo ubatizo katika Jina la Yesu Kristo si wa kweli. Nionyeshe kuzaliwa huku uliko nako, kufa. Na kama ungali una ulimwengu ndani yako, wewe ungali ni wa ulimwengu. Nionyeshe mambo haya. Haikubidi kuyahofia, yapeleke kwenye mashine ya kupimia. *Huu* hapa Mtambo wa Kupimia. Mnaona? Mnaona? Hiyo ni kweli.

160 Kwa hiyo wao wakasema, "Utaenda haidhuru." Ndipo kundi la ndugu wakamnyanyua juu, nalo lile joho likatoweka. Mnaona? Hivi Wapentekoste wasingekula hilo leo hii? Loo, jamani! Lilionekana kama kitu halisi, bali halikuwa ni kulingana na Neno.

161 Martin alisema Shetani alimtokea wakati mmoja, amevaa taji kubwa mno ya dhahabu, safu tatu ama nne za nyota ndani yake namna hiyo, zinang'aa na ni za kupendeza, jamaa mkubwa mno, mzuri, mwenye sura nzuri, amechanua nywele vizuri na kujinadhifisha, amevaa joho zuri mno, na viatu vyake miguuni

mwake vilikuwa ni dhahabu, akatokeza na kusema, "Martin, hivi unanifahamu?"

162 Sasa watu ambao hawayaoni maono, hili huenda lisininii—hili huenda lisininii. . .huenda msilifahamu, mnaona, lakini jinsi mambo huja kwako katika roho mbalimbali, na jinsi zilivyo danganyifu. Biblia ilisema wangewadanganya walio wateule kama yamkini, mnaona. Walio wateule, hao ni wale waliokusudiwa tangu zamani na kuzaliwa kwa ajili ya kusudi hilo. Mnaona? Mnaona?

163 Kwa hiyo akamjia mteule huyu, akasema, "Martin, hivi unanifahamu? Mimi ni Kristo." Akasema, "Utanitambua?" Ndipo Martin akasitasita. Lilionekana ni la kigeni. Akangoja dakika moja, kisha akasema tena, akasema, "Hivi hunioni mimi? Mimi ni Kristo. Unanitambua?" Akamwambia hivyo mara tatu au nne.

164 Kristo akasema, ama Martin akasema, "Shetani, ninakujua. Bwana wangu hajavikwa taji bado, bali watakatifu Wake watamvika taji." Hilo hapo Neno, likirejeshwa.

165 Hapo ndipo kanisa hilo la Kirumi lilipopata mafundisho mengi sana ya sharti, pepo waovu wakaingia, kinyume na Neno, nao iliwabidi kulikana Neno wapate kuyachukua mafundisho yao ya sharti na kuiondokea Biblia. Dumuni na Neno! Hiyo ndiyo kamba ya Uhai siku hizi. Kutakuwako na roho zitakazoinuka baada ya kitambo kidogo ambazo zitakidanganya kila kitu, karibu hivyo. Biblia ilisema hivyo. "Kama vile Yane na Yambre walivyoshindana na Musa, ndivyo watu hawa walioharibikiwa akili zao kuhusu ile Kweli," watafanya miujiza na kila namna ya ishara. Lakini dumuni na hilo Neno. Neno la Bwana lilimjia nabii, nao wakalileta, nasi tunawaamini manabii.

166 Angalieni, naam, yeye alisema, "Ninakujua, Shetani." Kasema, "Bwana wangu si mtu mkubwa namna hiyo. Bwana wangu aliondoka amevaa maskini vazi chakavu, akiwa na makovu ya misumari mkononi Mwake, bila kuvikwa taji, pamoja na vishungi vilivyojaa damu. Na hapo Yeye atakaporudi, Yeye atakuja jinsi hiyo, kwa kuwa Biblia ilisema Yeye atarudi jinsi hiyo hiyo alivyoondoka." Ndipo kitu hicho kikatoweka kutoka kwake. Loo, jamani!

167 Jinsi anavyoingia na kulifanya la kupendeza sana, "Loo, walinena kwa lugha. Hao ni—hao ni—hao ndio watu wazuri kuliko wote uliowahi kuona." Kamwe msiamini hilo. Iweni waangalifu.

168 Ninatumaini Neno haliwachoshi. Wakristo waliozaliwa hukua katika kimo cha Kristo wanapoendelea kuishi. Wanazaliwa tena, nayo maisha yao yanaanza kuumbika kama ya mtoto mchanga. Yanachukua umbo na kuanza kukua. Muda si muda wajua, hawa hapa katika kimo kikamilifu. Amina. Haya

basi. Siku baada ya siku, mwaka baada ya mwaka, wanakaa vivyo hivyo. Sasa rudini kwenye Neno, "Mkikaa ndani Yangu!"

169 Wao wanasema, "Nilizaliwa mara ya pili, haleluya, nilijiunga nao. Nilijiunga na *hili*. Nilijiunga. Sijui, mwaka jana niliamini katika Jina la Yesu, sasa ni—nimeliacha sasa, ni—ninaamini *hili*. Kweli niliamini ilikubidi kuishi, kuwa mtakatifu, bali mimi—mimi . . . *Nanii* anasema . . ." Wazururaji, wakitupwa huku na huku na kila wimbi la mafundisho. Mnaona? Haya basi.

170 Lakini zaliweni kwa Roho na mkue katika kimo cha Kristo! Unaliona, Ndugu Dauch? Kukua kukifikia kimo cha Kristo! Kupitia maisha yako, inathibitisha. Kama vile ikiwa ulizaliwa nabii, utabaki hivyo. Kama ulizaliwa Mkristo, utabaki hivyo. "Mkikaa ndani Yangu nayo Maneno Yangu yakae ndani yenu!" *Hili* linakukuza kukifikia kimo cha Kristo. Sio mwanasheria fulani mchanga akipigapiga, akipiga makelele, akilia, akikuambia *hili, lile, linginelo,* kusababisha mihemko mingi mno. bali mtu fulani ambaye amekua akafikia kimo cha Kristo, kote katika miaka amekolea na kuthibitishwa, akisimama usukani. Hakuna lingine! "Juu ya Kristo Mwamba wenye imara tunasimama, sakafu zingine zote ni mchanga udidimiao. Acha madhehebu na kanuni za imani zije, ziende, acha itikadi; nidumishe mnyenyekevu, Bwana, dumu moja kwa moja na Neno na usonge mbele moja kwa moja kupitia kwenye kijito. Yeye atatuongoza hata ufukoni." Kimo kikamilifu.

171 Sasa angalia, kama tukiona jinsi inavyotokea hapa, wala huwezi kubadilika baada ya mauti . . . Sasa wewe waangalie watu hawa wanaoingia, wanapata mihemko yote na kadhalika, wanakimbia nje na kesho wako *hivi*. Mmeliona? Mamia yao. Mnaona? Nanyi mnaona, m—mnaona kile kinachotukia. Na sasa vipi kama hao watu walikufa katika hali hiyo? Mauti hayalibadilishi.

172 Kwa hiyo, loo, enyi Wakristo, katika kufunga Maneno haya, hebu niseme hili. Hebu tumgeukie Yeye pamoja na Neno Lake, kwa uaminifu wote, tuje kwa unyenyekevu, kama Wakristo, na kuzaliwa mara ya pili kwa Roho Wake. Ndipo wakati unapozaliwa mara ya pili, unathibitishwa kuwa Mkristo kwa matunda unayozaa. Unalipata hilo, Dada Peckenpaugh? Wewe ni Mkristo kwa matunda unayozaa. "Kwa matunda yao mtawatambua." Hilo ni thibitisho. Huenda usizijue ABC zako, bali hata hivyo unaweza kuwa mama wa heshima, Mkristo. Huenda ukachukiwa na ulimwengu, (kama ukifanya hivyo kwa sababu ya kitu fulani ulichofanya, unachopaswa kuwa,) bali kama unachukiwa kwa sababu Yake, hiyo ni tofauti.

173 Huenda usi—huenda usiwe mwanatheolojia. Hebu mwangalie yule kipofu aliyezaliwa kipofu. Yesu alimponya. Alikuwa amezaliwa tangu kuzaliwa, hata hakuwa na mboni za macho. Naye Yesu akampa afya, akamponya. Ndipo mtu

huyo alipopata kuona, nao Mafarisayo wakamwuliza swali, kasema, "Huyo alikuwa ni Nani?" Wasingeweza kukana kwamba jambo fulani lilikuwa limetendeka. Sasa, mtu huyo hakuwa mwanatheolojia. Asingeweza kubishana kama vile wahubiri wangefanya, mbinu kidogo, asingeweza kuwaelezea. Yeye hakulijua Agano. Hakujua jinsi Masihi alikuwa azaliwe na kazi atakazofanya. Mtu huyo hakujua. Hakuwa mwanatheolojia. Lakini alifanya nini? Wao walisema, "Mpe Mungu sifa. Sisi ni wanatheolojia, nasi tunajua Yeye ni mwenye dhambi."

174 Sasa mtu huyo asingeweza kulikana neno lao, bali hivi ndivyo alivyosema, kwa maneno mengine, "Kama—kama Yeye ni mwenye dhambi na anafanya hili, basi mna shida gani ninyi jameni? Nyinyi nyote mna shida gani?" Mnaona? Akasema, "Kama Yeye ni mwenye dhambi, ama siye, sijui mimi, siwezi kusema hilo. Lakini jambo hili moja najua, ambapo wakati mmoja nilikuwa kipofu, sasa ninaona." Alikuwa akifanya nini? Yeye alithibitishwa. Hiyo ni kweli. Alikuwa akithibitishwa. Jambo fulani lilikuwa limetendeka kwake. Utu wake ulibadilishwa kutoka gizani kuingia nuruni, kutoka kipofu akapata kuona.

175 Naye mtu aliyezaliwa kwa Roho wa Mungu, ambaye wakati mmoja alikuwa na mfano wa utauwa, akikana Neno lake, na nguvu zake, na kusema, "Siku za miujiza zimepita," wakati akizaliwa mara ya pili, huenda asiwe ni mwanachuoni, huenda asiweze kulielezea Hilo, bali analiamini. Kama ninii . . .

176 Kama ndugu zangu weusi na dada hapa watanisamehe kwa kusema hili, maskini ndugu mwema mweusi huko Kusini, walisimulia hadithi yake ndogo, kasema alikuwa akibeba Biblia na hata asingaliweza kulisoma jina lake. Naye akasema "Mose, kwa nini unabeba hiyo Biblia?"

Akasema, "Ni Neno la Mungu."

Wao wakasema, vema, kasema, "Unaliamini Hilo?"

177 Akasema, "Naam, bwana, hakika ninaiamini." Kasema, "Ninaiamini kutoka 'chalada' hata 'chalada,' na ninaiamini 'chalada' pia, kwa sababu imeandikwa 'Biblia Takakatifu' juu Yake."

178 Kasema, "Unajuaje ni Biblia Takatifu?" Kasema, "Unajuaje ndivyo ilivyo?"

179 Akasema, "Ninaiamini tu. Hivyo tu." Hiyo tu ndiyo aliyopaswa kuwa nayo. Yeye aliiamini tu. Hakujua ni kwa nini, bali aliiamini.

180 Wakamwambia, "Mose, hivi wewe, ungefanya chochote ambacho Biblia hiyo ilisema ufanye?"

"Naam, bwana." Akasema, "Kama Biblia ilisema hivyo, ningelifanya." Haya basi.

181 Akasema, “Vema, Mose.” Akasema, “Sasa, vipi, kama ule uzio wa mawe pale, kama Bwana alikwambia uruke upitie kwenye ule uzio wa mawe, ungeruka, ungerukaje kupitia huo uzio wa mawe?”

182 Akasema, “Hivi Biblia inasema Mose aruke kupitia kwenye ule uzio wa mawe?”

183 Akasema, “Lakini vipi kama Mungu angesema nawe na kukwambia uruke kupitia kwenye ule uzio wa mawe?”

Akasema, “Kama ilikuwa ni Mungu, na Yeye aliniambia niruke, ningeruka.”

184 Akasema, “Utapitiaje kwenye huo uzio pasipokuwa na shimo ndani yake?”

185 Akasema “Kama ilikuwa ni Mungu, Yeye angekuwa na shimo pale wakati Mose afikapo pale.” Na hiyo ni kweli. Kweli!

186 Unathubutu kulichukua Neno la Mungu na kusimama pale na kusema ndivyo lilivyo! Hebu maskini mwanamke huyu hapa mwenye wasiwasi. Anafikiri atakufa, na kila kitu kingine ni shida kwake, mnaona. Hufi! Wasema, “Ninawezaje, Ndugu Branham?” Lichukue tu Neno Lake na usimame juu Yake wakati mmoja, unaona. Simama juu ya Neno hilo, uone kinachotukia. Mwambie ibilisi kwamba yeye ni mwongo. Umekuwa katika kukoma hedhi miaka hii yote, yapata umri wa miaka hamsini na saba. Basi kiondokee kitu hicho, ni ibilisi! Lichukue Neno la Mungu na kusema, “Kwa mapigo Yake mimi nimepona,” uone kitakachotukia. Ndipo utaacha kufikiria una mishtuko ya moyo na kadhalika. Huna mshtuko wowote wa moyo na upuuzi huo wote. Ni uongo. Huna. Liamini tu Neno la Mungu. Hiyo ni kweli.

187 Unapozaliwa mara ya pili, Mungu hukuthibitisha. Hivyo ndivyo Mungu anavyoyathibitisha maumbile yake yote. Kitu gani? Kwa matunda yao. Hivyo ndivyo anavyoithibitisha huduma Yake. Hiyo ni kweli. Watumishi Wake wote wanathibitishwa vile vile Yeye anavyoyathibitisha maumbile. Unajuaje kwamba ni mpichi? Kwa sababu huzaa mapichi. Unajuaje ni mtofaa? Unazaa matofaa. Unajuaje ni Mkristo? Ishara za Mkristo zinatoka kwake, maisha ya Kikristo yanatoka kwake. Unajuaje kwamba yeye ni mwalimu? Neno linatoka kwake. Unajuaje kwamba yeye ni nabii? Neno linakuja kupitia kwake, linashuhudia, thibitisho. Linajithibitisha lenyewe. Linakuwaje hivyo? Linapokufa na kuwa moja. Hiyo ni kweli. Tunapokufa na kuwa kiumbe kipya katika Kristo Yesu, linatuleta pamoja na wito wetu, tunadumu na wito wetu. Matunda ya Roho hutufuata tunapokuwa ni watumishi Wake. Tunapozaliwa mara ya pili, matunda ya Uzima wa Kristo hutufuata. Hiyo ni kweli. Unajuaje kwamba ni mpichi? Una mapichi. Unajuaje yeye ni Mkristo? Anatenda kama Kristo, anatembea kama Kristo, anazungumza kama Kristo, anaishi kama Kristo, juu ya dhambi, mshindi. Yeye hufanya nini,

kusema, "Mnaona nililofanya"? Kristo hakufanya hivyo. Yeye alimpa Baba sifa zote. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo mnavyojua hilo. Kwa matunda yao mtawatambua. Kile ambacho hakina budi. . .

188 "Amin, amin, nawaambia, mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi hata kuuelewa Ufalme wa Mungu."

189 Kwa hiyo sio ujumbe wangu wa Mwaka Mpya hapa saa sita na nusu, ama saa saba kasoro dakika ishirini, ila ushauri wangu ni kwako wewe, Mkristo, wewe unayempenda Mungu. Unapofikia kwenye madhabahu ya Mungu ya shaba ya hukumu, nawe unataka kuzaliwa mara ya pili, jilaze tu hapo juu. Usitarajie kuamka tena, utakufa. Huo ndio mwisho wako. Hivyo tu. Kama hufanyi hivyo, kama hujisikii kama unaweza kufanya hivyo, usifanye, usilijaribu, halitafaulu; kwa kilindi, kwa unyofu. Nikiwa na kama kurasa kumi zaidi za somo hili hapa, ama zaidi, Maandiko, ninaondoka. Lakini jilaze juu ya madhabahu ya Mungu ya shaba ya hukumu ya Mungu, na uwe mfu tu kabisa kwa ulimwengu kama Kristo alivyokuwa. Mnaona? Njoo ukiwa mfu tu kabisa kama vile yule nyoka aliyehukumiwa alivyokuwa katika bustani ya Edeni, alikuwa tayari amewakilishwa kwa mfano wa nyoka ya shaba, hakuna uhai hata kidogo ndani yake. Uhai wake wote ulikuwa umekwisha. Kristo alikuwa amekufa, walimwondoa msalabani na kumzika kaburini. Alikuwa—alikuwa amekufa. Ndipo basi akafufuka kwa ajili ya kuhesabiwa haki kwetu. Nasi tunakufa pamoja na Mwana-kondoo wetu madhabahuni, na kufufuka tena, kwa ajili. . .katika kuhesabiwa haki Kwake. Tunajuaje? Kwa sababu Uzima Wake uliomfufua Yeye kutoka kwenye hali hiyo ya mauti, Uzima ule ule hutufufua kutoka hali yetu ya kufa ya ulimwengu, ukatufanya kiumbe kipya katika Kristo Yesu, ndipo basi kwa Roho Mtakatifu tumetiwa muhuri katika Ufalme wa Mungu mpaka siku ya ukombozi wetu.

190 "Amin, amin, nawaambia, mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuelewa Ufalme wa Mungu." Usijaribu kulielewa. Kamwe hutaweza kulielewa. Yesu alisema usingeweza. Likubali tu, likubali tu kwa msingi wa Neno Lake.

191 Usiingie kiupofu sasa, na kusema, "Ee Bwana, nipe mhemko." Usifanye hivyo, "Bwana, nakwambia." La. Sema tu, "Bwana, niue, uondoe ulimwengu kutoka kwangu. Ni—ni—ningali ninayapenda mambo ya ulimwengu." Simaanishi uumbaji, kutua kwa jua na urembo, na vitu kama hivyo, hilo silo ninalozungumzia. Ninawazia juu ya tamaa mbaya, uchafu, utaratibu wa ulimwengu. Mambo haya yote ya ulimwengu. Ninii tu, yanakufa tu, yanakufa tu yenyewe, nawe huna. . . hayana mamlaka juu yako tena. Yanakuwa uvundo kwako, "Ah, kamwe sioni jinsi watu wanavyoishi ndani yake!" Unalia. Jinsi unavyozidi kuyaona, ndivyo unavyozidi kuwa mbaya! Naam, bwana. Huwezi kupatana nayo. Hakuna mahali pa kupatana.

Hakuna mahali pa kujiweka mwenyewe mle ndani wakati kukiwako na ulimwengu mle ndani. Umeyafia mambo hayo. Nawe unawezaje, ukiisha kufa kwa ulimwengu, kisha ujihusishe katika mambo yake tena? Huwezi kufanya hivyo. Kwa hivyo usifanye hivyo. Yafie mambo ya ulimwengu.

192 Bwana awabariki. Iweni Wakristo waliozaliwa mara ya pili. Zaliweni mara ya pili, ndipo haitawabidi kusema, "Ndilo jambo lililo gumu kuliko yote," ninyi wanawake, "kwangu kuachilia nywele zangu zikue." "Ndilo jambo lililo gumu kuliko yote kwangu kuachana na hasira yangu," wewe mwanamume. "Jamani, sina budi kumwambia tu mke wangu. Nikimpata, jamani, na kumtikisa na kusema, 'Ninajua mimi ni Mkristo, sipaswi kufanya hivi, bali wewe nyamaza na uketi chini.'" Ha-aha, usifanye hivyo. Unaona?

193 Ungetaka kuona wakati ungeweza kumkumbatia, useme, "Mpenzi, hilo halimfai Mkristo." Hivyo ndivyo unavyotaka kuwa, sivyo? Unaweza kuwa hivyo. Mnaona? Na wakati mtu anapokupiga kofi upande mmoja wa uso, haikubidi kumkata kwa kisu cha mfukoni. Unaona? Mtu akikupiga kofi upande mmoja wa uso, sema, "Ndugu, kwa nini ukafanya hivyo?" Unaona? Haya basi. Huo ni Ukristo. Mtu anaposema jambo fulani ovu kukuhusu, badala ya kujaribu kulifanya tamasha kubwa, nenda kisiri mahali fulani useme, "Baba wa Mbinguni, huyo mtu ni mwanadamu. Ninaomba ya kwamba utaiondoa roho hiyo kwake. Usimwache afanye hivyo. Ninaomba uyaokoe maisha yake."

194 Usiseme, "Bwana, ninajua sipaswi kusema hilo." Vema, huenda usiliseme kwa midomo yako, bali ulimaanishe moyoni mwako. Unaona? Moyo wako ndio ulio muhimu, unaona. Unapozaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, kweli unampenda kila mtu. Sasa huzipendi njia zao na vitu kama hivyo, hutaki kuvishiriki. La, bwana. Kaa mbali na mambo ya ulimwengu, bali ujiweke bila waa. Na jinsi tu inavyokubidi kufanya hilo, linatoka ndani likienda nje, kama vile hua akiyatengeneza manyoya yake, mnaona. Haimbidi kuyatengeneza, aseme, "Sasa, leo sina budi kuyapangusa yote haya," halafu namna hiyo. La, yeye ana mafuta ndani yake kwa kuwa yeye ni hua, yanamdumisha tu safi. Mnaona? Hiyo ni kweli.

195 Hivi hamtafanya hivyo? Hivi hamtampokea jinsi hiyo? Huo ndio ushawishi wangu kwenu kwenye Mkesha huu wa Mwaka Mpya. Ninashawishi maskini maskani haya. Jinsi ninavyowapenda, jinsi ninavyolipenda kundi hili dogo la watu! Jinsi ningetaka kuingia wakati mmoja, nishuke nitembee kupitia humu jengoni, na kuangalia tu. Mnajua yale sikuzote nimetamani kuona? Kanisa lililojazwa na Roho, ambalo dhambi hata haingeweza kulikaribia. Mara mshiriki mmoja akifanya kosa, Roho angaliitambua mara moja. Angeogopa kujiunga na

Wakristo kabla hajaikiri na kuisahihisha, kwa sababu angeitwa mara moja mkutanoni mnapokutana pamoja. Mnaona hapo, hilo si lingekuwa ni la kupendeza? Ndipo aliye mchafu anaingia na kuketi miongoni mwenu, muda si muda mwajua, Roho Mtakatifu ananena kwa njia ambayo inazifunua siri za moyo wao, mnaona, kuwaambia. Sasa, kama litafanya kazi kwa mmoja, litafanya kwa huyo mwingine. Mnaona? Mnaona? Na kila mtu katika maombi, ninyi nyote kwa umoja, mtu mmoja, mtu mmoja tu, kama vile sote tulivyo washiriki wa Mwili huu tukienda moja kwa moja, sote tumezaliwa mara ya pili kwa Roho wa Mungu, tukajazwa na Roho yeye yule, tukabatizwa kuwa Mwili ule ule. Hilo si lingekuwa ni ajabu? Sasa, tunaweza kuwa nalo, Mungu alituahidi hilo. Lakini kwanza, kifo, kuzikwa, na kufufuka pamoja Naye.

196 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa ajili ya maombi. Kunazo leso zilizowekwa hapa pia.

197 Mungu mtakatifu, tunatambua, Bwana, ya kwamba... utakatifu wa kusimama mahali hapa. Tunatambua kwamba tuko katika Nyumba ya Mungu. Tuko ndani, tukishiriki pamoja na Mwili wa Kristo, ambao ni Nyumba ya Mungu. Washiriki wa huu Mwili wamekusanyika pamoja. Kuna mmoja anayetoka mahali pamoja, na mmoja pengine, wakikusanyika pamoja. Na leo hii, kwenye somo hili la shule ya Jumapili, limekuwa ndefu na kurefushwa. Lakini, Baba, ninaamini ya kwamba limekusudiwa na Wewe, ya kwamba linapaswa kuwa hivi, ili tuweze kuelewa kile kuzaliwa na ufufuo yanavyomaanisha. Maana ya kuzaliwa mara ya pili. Hatuna budi, mambo ya kwanza yatangulie, ni lazima tufe kusudi tuzaliwe mara ya pili. Wewe kamwe huzibadilishi Sheria Zako. Kanuni ya maumbile ingali inasimama. Kanuni ya maumbile ni kwamba kila mbegu haina budi kufa kwanza ili iweze kuzaliwa tena. Nasi tunatambua ya kwamba sisi, pia, hatuna budi kufa kusudi tuzaliwe mara ya pili. Na wengi sana, Bwana, leo hii, ninaomba ya kwamba utusamehe, wengi sana wametegemea ujuzi fulani waliokuwa nao, hata wanadai wamezaliwa mara ya pili. Lakini matunda ya maisha yao yanaonyesha ya kwamba ni... walikuzwa kwenye mti usiofaa.

198 Hiyo ilikuwa ndiyo sababu yangu, Baba, asubuhi ya leo kuuliza kama Ndugu Neville alinena nami kuuleta Ujumbe, ningefundisha tu shule ya Jumapili. Na kwa hiyo, Baba, nimelifanya kwa—kwa upendo na kwa moyo wangu wote, ili watu waweze kujua hilo, sio kutegemea maskini ujuzi fulani waliokuwa nao, bali kutulia kwa uchaji juu ya maisha yao ya kila siku; jinsi wanavyoishi katika nyakati zile wamo kanisani, na jinsi wanavyoishi wakati ma—majaribu makubwa yanapokuja huko nje. Wanakimbia Msalabani wapate msaada wakati shida zinapotokea, ama wanatembea katika roho yao wenyewe na mawazo yao wenyewe? Wanakasirisha wakati

wanapokasirishwa? Hilo ndilo swali hili, Baba. Basi tunapoona ya kwamba haiwezekani kabisa kwa yeyote wetu kumwokoa mwenziwe, kwamba Mungu ameweka njia iliyotengwa, Dhabihu i—itoshelezayo kwa yote, na Hiyo ndiyo Njia pekee tunayoweza kuijia. Sio kwa kanisa lolote, kanuni yoyote, dhehebu lolote, mhemko wowote, bali kwa njia ya Kristo. Kama vile mtu wa kwanza, yule mwenye haki alikufa, alikufa madhabahuni pamoja na mwana-kondoo wake. Na kufikia saa ii hii, mtu yeyote mwingine mwenye haki hana budi kufa kwenye madhabahu ya shaba ya Mungu, pamoja na Mwana-kondoo wake, Kristo Yesu. Ndipo tunakufa pamoja na Yeye, na kufufuka upya, katika Maisha mapya. Tujalie, Bwana, kwamba halitaukosa moyo wowote hapa ndani.

199 Hebu na tuliwazie tena leo hii, Bwana, tunaporudi alasiri ya leo, tena saa moja na nusu, kuanzisha hapa mfululizo wa mikutano katika mahubiri usiku wa leo. Ninaomba ya kwamba Wewe utambariki kila mmoja wa watumishi Wako usiku wa leo kwa Jumbe zenye nguvu, Bwana. Tujalie. Jalia mioyo yetu ijazwe. Watu hawa walioendesha motokaa kutoka mbali kuja huku, jalia . . . wajazwe sana na Injili ya nguvu za Mungu kupitia mkesha wa huu Mwaka Mpya hata wataondoka kutoka hapa wakifurahi na kushangilia. Wajalie, Bwana, ukiwapa Chakula cha kiroho kwa ajili ya mwaka ujao. Tujalie.

200 Tusamehe makosa yetu, kama tunavyowasamehe wale wanaotukosea. Pia Wewe ulisema, "Iwapo kutoka moyoni mwako humsamehe kila mtu makosa yake, wala na Baba yako aliye Mbinguni hatakusamehe." Kwa hiyo, Bwana, tunamsamehe kila mtu. Sisi, kwa imani, asubuhi ya leo, tunaziweka nafsi zetu juu ya madhabahu, teketeza kila chembe ya maisha ya ulimwengu kituondokee, Bwana. Jalia moshi upande juu kutoka kwenye dhabihu yetu, Bwana, na iwe manukato yenye harufu nzuri puani Mwako. Tujalie, Bwana, kwa kuwa hatuweki mwana-kondoo aliyeteketezwa, bali tunajiweka wenyewe huko juu kama wenye dhambi, tupate kuteketezwa kama wenye dhambi, na kubadilishwa kuwa wana-kondoo wa kuzaliwa upya. Tujalie, Bwana.

201 Kisha usituongoze majaribuni, bali utuokoe na uovu; uovu wa maradhi, uovu wa kukandamizwa. Mponye kila mmoja aliye kwenye jengo hili asubuhi ya leo. Kila mgonjwa apate kuponywa leo, Bwana. Ninanena maneno haya katika Jina la Bwana Yesu, kwamba milima iliyo mbele za watu ipate kuondolewa yote leo hii. Kama ni maradhi, kama ni tamaa mbaya, kama ni hamaki, kama ni kitu chochote cha ulimwenguni, jalia kiondoke njiani nalo Neno la Mungu liingie ndani na kudhihirishwa maishani mwao. Utuokoe na uovu; kwa kuwa Ufalme ni Wako, Bwana, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza

Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Sasa peaneni mikono.

Nampenda, na-. . .

Geuka tu moja kwa moja, useme, "Salamu, ndugu yangu, salamu!"

Kwani alinipenda kwanza
Na kununua wokovu wangu
Mtini Kalvari.

Endelea tu kucheza.

202 Ninataka kumshukuru kila mmoja wenu kwa ajili ya wema wenu mwaka huu uliopita. Labda nitaupata Ujumbe wangu usiku wa leo, Bwana akipenda, saa moja na nusu. Ninataka kumshukuru Charlie na Nellie, na Rodney na mke wake, kwa ajili ya wema wao, ule msimu wa kuwinda niliokuwa kule chini, walinikaribisha kana kwamba nilikuwa baba yao ama ndugu yao. Na kwenu ninyi watu wote ambao mmekuwa wakarimu sana kwangu, asanteni. Ndugu na Dada Dauch, na Ndugu Wright, pia Ndugu Ben, na wengi, ninyi watu wo—wote, Ndugu Palmer na, mwajua, ninyi nyote kutoka Georgia, kotekote kila mahali, asanteni.

203 Jambo lingine, baba ya Margie, walipiga simu jana na kusema alikuwa ni mgonjwa. Margie na Rodney wa—wako hapa? Hawako? Huyo mzee ana hali gani? [Ndugu kwenye kusanyiko anasema, "Huenda ana nafuu tu kidogo."—Mh.]

Hebu tu, polepole, hebu tuombe.

204 Baba wa Mbinguni, majuma machache yaliyopita niliketi kwenye baraza ndogo ya mashambani huko juu sana barabarani kule Kentucky. Baba mzee aliketi hapo nje amevaa ovaroli, na shati lake la samawati lililopauka, akitetemeka. Nikamshika mkono na kuona kwamba alikuwa anakaribia mwisho wake. Maskini mama kizee akanialika ndani nikale biskuti chache na supu. Bwana, walikuwa tu wakiliheshimu Neno Lako. Sasa yeye karibu hayuko hapa, anatuacha. Usimwache afe mwenye dhambi, Bwana. Labda imekuwa ni ninii yetu. . . Kosa, la mtumishi Wako, Bwana. Maskini mzee huyo, bila kujua kitu ila akilima udongo na kuwapatia watoto wake riziki, bali nilimwona ana roho nzuri nyenyekevu. Usimwache afe mwenye dhambi. Binti yake ni mmoja wetu, Bwana. Na jinsi maskini Margie, hayo mabega madogo yakiuma, na jinsi alivyonihudumia na kujaribu kunitengenezea kitanda nipate kulalia huko chini, ki—kiamshakinywa mezani, na yeye na Nellie na Charlie na hao wote, mama Cox. "Naye alikuwa akilia," walisema, "kwenye simu. Baba yake anaondoka." Huyo ni baba yake.

205 Bwana, njoo kwenye kihema hicho cha oksijeni sasa, usibishe kwenye hicho kihema, bali kihema kile cha mlango wa moyo wake. Labda baadhi yetu hatujatimiza jukumu letu kumwendea, Bwana. Baadhi ya watumishi Wako wengine, labda katika siku za ujana wake wakati akili yake ilikuwa makini, labda ni kosa letu, Bwana, kwamba hatukumshawishi. Basi tusamehe, Bwana, na umpeleke katika Ufalme Wako. Lijalie, Baba. Tunamkabidhi Kwako sasa. Na kama yawezekana, ama uwe ni mpango Wako mkuu, kama utamwinua, Bwana, labda baadhi yetu tutakuwa na nafasi ya kuzungumza naye. Hata hivyo, ombi letu ni kwa ajili ya nafsi yake, Bwana, maana itafanya safari yake hivi karibuni sana, inaonekana hivyo, ikiabiri kwenda huko ng'ambo kusikojulikana, loo, pasipo na rubani, bila mtu wa kumwongoza kupitia kwenye ukungu na umande huko ng'ambo. Atapotea njia, Bwana. Jalia Rubani anayeijua njia, amjie asubuhi ya leo, aitie nanga meli yake ndogo kando ya ile meli ya kale ya Sayuni. Wakati atakapoanza safari yake, atakuwa na hakika kufika salama. Tujalie, Baba. Tunamkabidhi Kwako sasa, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

> Nampenda, nampenda

Hebu tuinue mikono yetu.

> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

206 Usiku wa leo nitajaribu kuharakisha Ujumbe kidogo, kama nilivyofanya asubuhi ya leo. Sasa ponyokeni mwondoke. Laiti ningaliweza kwenda nanyi nyote nyumbani, niwape nyote chakula kizuri cha kutwa. Hakika ningefanya hivyo kama ningeweza. Bali natumaini kwamba Bwana atawapa cha—chakula halisi, tukinena kiroho, katika wema na rehema Zake, mpate kuliona na kukua mkifikie kimo Chake kikamilifu hata mumpendaye, Mwakozi wenu, Yesu Kristo. Sasa tunapoondoka humu jengoni, na kusimama kwa ajili ya maombi, ya kupumukana, tunataka kuimba wimbo wetu, na mwe na hakika mtautii, *Peleka Jina la Yesu*. [Ndugu Neville anasema, "Ninalo tangazo ninalotaka kufanya."—Mh.] (Ati nini? Wewe nenda uliruhusu kusanyiko kuondoka.) Sasa, tutafanya tangazo katika dakika moja, tunalo tangazo mara baada ya kuuimba wimbo wetu. Vema.

> Peleka Jina la Yesu,
> Mtoto wa huzuni na majonzi;
> Litakupa furaha na faraja,
> Lipeleke kila uendako.
>
> Jina la thamani, Ee jinsi lilivyo tamu!
> Tumaini la duniani na furaha ya . . .

Bwana Yesu, waponye watu hawa, ninaomba, katika Jina la Yesu.

Tumaini la duniani na furaha ya . . .

Peleka Jina la Yesu,
Kama ngao dhidi ya kila mtego; (Sikilizeni sasa, nini?)
Majaribu yakikuzunguka, (Unafanya nini?)
Litamke tu hilo Jina katika maombi.

Jina la thamani, Ee jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni;
Jina la thamani (Jina la thamani!), Loo jinsi lilivyo tamu!
Tumaini la duniani na furaha ya Mbinguni.

207 Sasa, kumbukeni, ninaamini ya kwamba Yesu Kristo anasema hili kwa kila mwanadamu, kwenye Fundisho Lake la kwanza: "Mtu asipozaliwa kwa maji," hilo ni Neno, kuoshwa kwa maji kwa Neno, "na kwa Roho," ambaye ni Roho Mtakatifu, Roho Mtakatifu akilithibitisha Neno, "hawezi kuuona Ufalme wa Mbinguni." Mnaamini hilo? Mnaona? "Kwa maji," kuoshwa kwa maji kwa Neno, Neno na Kweli, Yeye ndiye Kweli, "maji na Roho," Roho akija pamoja na Neno, kulithibitisha Neno, likimfanya Mungu aishi ndani yangu, mnaona, "hatuwezi kuufahamu Ufalme wa Mbinguni mpaka hilo limetukia," ndipo hilo linapoanza kutukia, kwamba tunaliona Neno ndani Yetu, tumezaliwa kwa Neno na kwa Roho, likijidhihirisha Lenyewe, likiniongoza, sio *kuniondoa* kwenye Neno, Roho huniongoza *kwenye* Neno, nalo Neno likiishi ndani yangu, likimfanya Mungu adhihirike katika maisha yako, "kamwe hutaufahamu Ufalme wa Mungu, wala kamwe huwezi kuingia humo." Mungu awabariki.

Ndugu Neville.

61-1231M Huna Budi Kuzaliwa Mara Ya Pili
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org